epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Ijumaa Desemba 27, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581903
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
Nipashe digital 0677 020 710 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 2
**Bashungwa** asisitiza kudumisha tunu amani



UKURASA WA 4
**Mtoto** adaiwa kuuawa wakati wazazi wakiwa matembezini

UKURASA WA 4
**Atoroka** kwa mumewe madai ya kunyanyaswa



**SLOT: HATUDHARAU KLABU YOYOTE EPL** UKURASA 21

# Askofu awajia juu viongozi kujikweza

• **Awataka** kutumikia watu, si kutumikiwa, Malasusa ahimiza malezi bora kwa watoto... *Endelea Ukurasa 2*



Askofu George



Askofu Alex Malasusa



## Kanisa lapongeza serikali ujenzi wa miradi kimkakati

UKURASA 3

# Watu 12 wafariki dunia kwa ajali wakati Krismasi

UK. 3

**MICHEZO** **CAF YAIBEBA SIMBA TUNISIA** UK.24

**MAONI,** UK.6



Wananchi wakimpakia dereva wa bodaboda kwenye gari la wagonjwa mara baada ya kugongwa na gari aina ya Kluger yenye namba za usajili T.199 DZF maeneo ya Makaburi Ndembezi Manispaa ya Shinyanga jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Askofu Okoth awajia juu viongozi wanaojikweza

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mara, George Okoth, amewataka viongozi wa serikali, siasa, dini na kimila kuacha kujikweza na kujiinua bali wawe wanyenyekevu na kuihudumia jamii ipasavyo.

Askofu Okoth alisema hayo jana katika ibada ya shukrani ya Sikukuu ya Kuzaliwa kwa Kristo (Krismasi), maarufu kama 'Boxing Day' iliyofanyika mjini Musoma hapa.

Alisema viongozi wa ngazi zote wanatakiwa kuiga mfano wa Yesu Kristo ambaye alikuja na dhana ya tofauti katika utawala, akijifanya mtu anayewatumikia watu na wala si watu kumtumikia yeye.

"Yeye anataka kiongozi ajione kama mtumishi anayetumika kwa ajili ya watu wengine, si kutumika kwa ajili ya maslahi yake ambapo watu watahamisha mawazo yao kuwaona kwamba viongozi ni watu wakubwa, mabosi pia wako tofauti na wao," alisema Askofu Okoth.

Alisema jamii wanayoitumikia ndiyo iliwapa kibali cha kuwa viongozi kutokana na asilimia kubwa wanapigiwa kura na wananchi, hivyo kuwataka kuwa na utii kwa kuwasikiliza na kuwahudumia bila kujikweza.

**AKEMEA UKATILI**

Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Tanzania Missionary Revival (TMRC), Jacob Lutubija, aliwataka waamini wa kanisa hilo kuacha vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na wanawake aliwataka kushiriki kikamilifu kudhibiti vitendo hivyo.

Alisema kuishi kwa kumtegemea Mungu husaidia kuondoa vitendo vya ukeketaji na ndoa za utotoni kwa jamii.

"Ukeketaji umeshamiri katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wetu wa Mara, wazazi kuchukua mahari kwa mtoto ambae hajafika umri wa kuolewa na kukatishia masomo,uvutaji bhangi na madawa ya kulevya mambo haya maovu hata kwenye jamii hayapendezi"alisema.

Alisema mbali ya kunywa na kula vyakula vizuri katika sherehe hiyo, aliwataka waumini kumruhusu Yesu azaliwe katika mioyo yao aweze kileta amani huku akitoa wito kwa jamii kutoendelea kukumbatia imani potofu na kuishi maisha yenye hofu ya Mungu.

Mwinjilisti wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Victoria (DVN), Sylvester Mhamaka, aliwataka wazazi kutambua jukumu lao la malezi kwa watoto ili kukabiliana na mmomonyoko wa maadili.

Alisema Mungu alimleta Yesu duniani ili kurudisha uhai wa mwanadamu kwa kuwa kiongozi katika maisha yake.

Alisema maadili katika jamii yamebadilika wazazi wameshindwa kuwa karibu na vijana na mabinti zao ambao wanajifunza mambo maovu kwenye mitandao kupitia simu janja hali inayochangia kuwepo kwa vitendo vya usagaji na ushoga.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Bashungwa asisitiza amani, upendo, umoja

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Innocent Bashungwa, ameomba Watanzania kuendelea kutunza tunu za upendo, umoja, amani na kufanya matendo ya huruma.

Bashungwa alitoa kauli hiyo juzi alipoungana na waumini wa Kanisa Katoliki Parokia ya Kiruma katika ibada ya Krismasi.

Waziri Bashungwa alisema serikali itaendelea kushirikiana na taasisi za dini katika kufundisha wananchi kuishi kwa upendo na amani.

"Tukipendana tutakuwa wamoja, tutakuwa na amani, na tutadumisha tunu zetu ikiwamo ya ujirani mwema na kufanya matendo ya huruma," alisema.

Awali, Paroko Msaidizi wa Parokia ya Kiruma, Padre Salapion Mberwa, aliwahimiza waumini wa kanisa hilo, kudumisha upendo na amani.

"Mahali penye upendo kuna umoja. Tusherehekee sikukuu hii kwa kuenzi upendo na umoja kwa sababu mahali penye umoja ndipo penye amani,"alisema Padre Mberwa.

Juzi katika sehemu ya salamu zake za Sikukuu ya Krismasi, Rais Samia Suluhu Hassan, aliwakumbusha Watanzania juu ya upendo kwa ndugu na jirani, juu ya uzalendo kwa taifa na kuishi katika kweli.

Kadhalika, aliwakumbusha juu ya unyenyekevu hasa wanapojaliwa nafasi za kuwatumikia wengine, kuwa na shukrani ikiwamo kuungana kwa pamoja kuiombea nchi ili iendelee kudumu katika amani, umoja na utulivu.

Rais Samia aliwataka kusherehekea sikukuu hiyo kwa kujumuika na familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa furaha na upendo na kutaka historia ya Yesu Kristo iwape tafakari juu ya mwanzo mpya katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

# Malasusa ahimiza wazazi malezi bora kwa watoto

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa, amewahimiza wazazi na walezi kuwalea watoto wao katika misingi ya dini ili wakue na kuimarika kiimani baada ya kupata sakramenti ya Kipaimara.

Askofu Dk. Malasusa alisema hayo jana kwenye ibada ya kuwakumbuka wafia dini iliyofanyika KKKT Usharika wa Mbezi Beach, Dar es Salaam ambayo iliambatana na sakramenti ya kipaimara na ubatizo.

Aliagiza viongozi wa kanisa kuendelea kutoa elimu ya misingi ya kiimani kwa vijana hao ili wasiache njia ya imani yao.

"Mnaposali hakikisheni wanafunzi hawa waliopata mafundisho ya kipaimara mnaendelea kuwapatia elimu ya misingi ya kiimani ili wasiache njia ya imani yao.

"Tunataka wanafunzi hawa waendelee kumtumikia Mungu na kuishi maisha ya imani walivyojifunza," alisema.

Juzi akihubiri katika ibada ya Krismasi, katika Kanisa Kuu la Azania Front, Askofu Malasusa alionesha kusikitishwa na vijana kuwa nyuma katika suala la imani tofauti na ilivyo katika makundi mengine.

Alisema vijana wengi wakipata sakramenti muhimu wamekuwa hawana mwendelezo mzuri wa imani yao. "Kwenye sakramenti kama hizi za kipaimara, huwa tunakuwa na vijana wengi, lakini baada ya hapo wengi huwa hawaonekani kanisani, ni vema kuendelea kuwafundisha vijana wetu kumpenda Mungu na kuwa watu wa imani," alisema.

Akihubiri katika ibada hiyo, Askofu wa Kanisa la Morovian Jimbo la Mashariki, Lawi Mwankuga, aliwataka Wakristo kuwa waamini katika kila jambo hasa katika mazingira ambayo wengine wanaweza kushindwa kuwa waaminifu.

"Mwenyezi Mungu atupe neema hata pale ambapo wengine wanaweza wakashindwa kuwa waaminifu, atujalie tuwe waaminifu, asubuhi, mchana na jioni, wewe wajibika kwa ajili ya taifa zima la Tanzania,"alisema Askofu Mwankuga.

Katika ibada hiyo,wanafunzi 30 wa usharika huo wa KKKT Mbezi Beach,walipatiwa sakramenti ya kipaimara.


IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.29094 OF 2024

IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE

MABULA TAWA KIKOME--------DECEASED

AND

IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY

1. MAHADI TAWA KIKOME--------PETITIONER
2. ..........................................

GENERAL CITATION

(Under Rule 75 of Probate Rules and any other enabling Provision of the Law)

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner. Objection to the grant should be filed on or before the 27th day of DECEMBER, 2024.

**Dated at Morogoro this 03RD day of DECEMBER,2024.**

PRINCIPAL/ SENIOR/ RESIDENT MAGISTRATE
MOROGORO DISTRICT COURT



KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

MIRAJI MBARAKA KIBUNDA

Anatangaza kupotea kwa kadi za Pikipiki

Zote aina ya Fekon zenye Usajili

**MC 924 CUZ, MC 716 CUT na MC 332 CUA**

Kwa yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu nae.

TAARIFA YA POLISI:**PHQ/TAN/LUS/14088/2024**

## HABARI KITAIFA



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake Jinsia na Wanawake na Makundi Maalum, (anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii na Makundi Maalum), Wakili Amon Mpanju akikabidhi zawadi mbalimbali kwa watoto wanaolelewa Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini Dar es Salaam kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan juzi. **PICHA: RAYMOND ISHENGOMA**

# Ajali zaua watu 12 wakati wa Krismasi

**Na Waandishi Wetu**

WATU 12 wamefariki dunia kwa ajali za magari na wengine kujeruhiwa wakati wa Sikukuu ya Krismasi katika mikoa ya Tanga na Lindi.

Mkoani Tanga, ajali ya gari iliyotokea juzi saa 3:00 usiku, watu 11 walifariki dunia na wengine 13 kujeruhiwa baada ya lori aina ya Mitsubishi Fuso lililokuwa likitokea Lushoto kwenda Dar es Salaam, kugongana na basi dogo aina ya Toyota Coaster lililokuwa likitokea Mkata kwenda jijini Tanga.

Ajali hiyo ilitokea ikiwa ni siku moja baada ya Desemba 25, mwaka huu, majira ya saa 12:00 asubuhi katika barabara ya Chalinze - Segera na watu wanane kufariki dunia papo hapo na wengine 8 kujeruhiwa baada ya magari mawili kugongana uso kwa uso. Ajali hiyo ilihusisha lori la mizigo lenye Usajili T 707 EBZ na basi dogo aina ya Toyota Coaster lenye Usajili T 497 DZW.

Juhudi za kumtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Almachius Muchunguzi, ziligonga mwamba kutokana na simu zake kutokupatikana.

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Wakili Albert Msando, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo apokariri wa na vyombo ya habari jijini Tanga.

"Watu 11 wamefariki dunia, wakiwamo madereva wa magari yote mawili na majeruhi 13 wamepelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni kwa ajili ya kupata huduma ya matibabu. Kati yao, majeruhi tisa hali zao si nzuri na madaktari wanaendelea na juhudi za matibabu", alisema Msando katika taarifa hiyo.

MWINGINE LINDI

Mtu mmoja amefariki dunia na wengine saba wakazi wa Kigamboni, Dar es Salaam wamepalekwa katika Hospitali ya Mkoa wa Lindi Sokoine kwa matibabu, baada ya gari walilokuwa wakisafiria kwenda kijiji na kata ya Ng'apa mkoani Lindi kupata ajali na kupinduka.

Kwa mujibu wa maelezo kutoka kwa baadhi ya majeruhi hao na kuthibitishwa na uongozi wa Hosptali na Jeshi la Polisi, ajali hiyo ilitokea juzi eneo la Machole Manispaa ya Lindi saa 3:00 usiku.

Wakizungumzia ajali ilivyotokea, baadhi ya majeruhi hao, Tabu Mchapo, Rahma Abdallah na Rukia Issa, walisema walikuwa wanatoka Dar es Saalam kwenda kijijini kwao Ng'apa kwa ajili ya kusheherekea Krismasi na Mwaka Mpya.

Majeruhi hao walisema wakiwa wanasafiri na gari lao binafsi aina ya Toyota Noah (bila kutaja namba zake) likiendeshwa na kaka yao, Selemani Panuli, walipofika eneo la Machole mbele yao waliona mwanga mkali na kupoteza mwelekeo kaka yao na kupinduka.

"Mimi nilikaa mbele na kuona mwanga mkali lakini si wa magari wala pikipiki na kuzimika kisha gari ikajipiga na kupinduka zaidi ya mara tatu na kusimama," alisema Tabu.

Alisema baada ya gari kutulia, dereva alikuwa ametoka kwenye kiti chake na kichwa chake kulala juu ya miguu yake bila kumtambua kwamba alikuwa tayari ameshafariki dunia.

Tabu aliyeumia kichwani alisema wakiwa wanahangaika kujaribu kujiokoa, lilipita gari la halmashauri na kuwapa msaada wa kufikishwa Hosptali ya rufani ya Mkoa ya Sokoine kupatiwa matibabu.

"Ndani ya gari tulikuwa watu wanane na watoto wetu wanne tukienda kwetu Ng'apa kula sikukuu ya Mwaka Mpya," alisema Tabu.

Rahma, aliyevunjika mkono wa kushoto, alisema alikuwa amekaa nyuma na kumpakata mtoto. Alisema baada ya mwanga huo kupotea, giza nene lilijitokeza na kusababisha dereva apoteze mwelekeo na kupinduka huku wengine wakichomoka na kutupwa nje.

Hassan Lukanda, Muuguzi Wodi Na. 4 walikolazwa majeruhi hao, alisema walipokea majeruhi hao saa 5:0 usiku na kwamba hali zao zilikuwa zinaendelea kuimarika kutokana na tiba wanazozipata katika hospitali hiyo.

Somoe Mnumba, mhudumu chumba cha kuhifadhia maiti, alisema akiwa nyumbani saa 5:30 usiku, alipigiwa simu kwa ajili ya kuchukua mwili wa Panuli kwa ajili ya kuuhifadhi.

Akizungumza kwa niaba ya Mganga Mfawidhi wa Hosptali hiyo, Dk. Alexander Makalla, Ofisa Habari na Uhusiano wa wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi ya Sokoine, Pendo Mustapher, alisema walipokea majeruhi saba bila kutaja majina wakiwamo watoto wanne kati yao watatu wanawake na mwanamume mmoja.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) John Imori, alikiri kutokea kwa ajali hiyo huku akiwataka madereva kuwa makini wanapokuwa wanaendesha vyombo vya moto ili kuepuka ajali.

"Ni kweli taarifa ya ajali hiyo ninayo lakini nashindwa kuelezea kwa urefu kwani niko nje ya ofisi," alisema Imori.

**-Imeandikwa na Boniface Gideon (Handeni) na Saidi Hamdani (LINDI)**

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*






# Serikali yapongezwa ujenzi miradi kimkakati

**Zuhura Zukheri Na Francis Godwin,** IRINGA

MAKAMU Mwenyekiti wa Makanisa ya Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) Mkoa wa Iringa, Askofu Dk. Blasston Gaville, ameipongeza serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya kimkakati.

Dk. Gaville ambaye ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Iringa, alisema hayo juzi wakati akitoa salamu za Krismasi baada ya ibada ya kitaifa ya Krismasi iliyofanyika katika Kanisa Kuu la KKKT Dayosisi ya Iringa, mjini hapa.

Alisema CCT na waumini kwa ujumla wanaipongeza serikali kwa kazi kubwa zinazofanyika, zinazoonekana na hata zile zisizoonekana kwa macho ya kawaida.

Askofu Dk. Gaville alisema miradi mikubwa ya kimkakati kama ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma na uendelezaji wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Julius Nyerere ni mfano mzuri wa juhudi hizo.

Pia, aliipongeza Serikali kwa kuzindua vifurushi vipya vya bima ya afya kwa makundi mbalimbali, hatua inayolenga kuboresha afya za Watanzania wengi.

"Watanzania wenzangu, huu ni wakati wa kumwombea Rais wetu na serikali yake kwa ujumla. Utekelezaji huu wa miradi tunaouona haujafanyika kwa muda mrefu nchini. Hii ni fursa ya kuimarisha maendeleo na afya ya wananchi wetu," alisema.

Askofu Dk. Gaville pia alisisitiza umuhimu wa kulinda na kutunza miradi hiyo, huku akiwataka Wakristo na Watanzania kwa ujumla kutumbua mchango wa serikali katika kukuza sekta za elimu, afya, na uwekezaji wa kimkakati.

Pia aliwapongeza Watanzania wote walioshiriki kikamilifu katika uchaguzi wa serikali za mitaa kwa amani, akiwahimiza wale waliokosa nafasi za uongozi kushirikiana na viongozi waliochaguliwa ili kudumisha amani na maendeleo ya taifa.

Dk. Gaville pia aliwakumbusha Watanzania juu ya changamoto za hali ya hewa, akiwataka wakulima kutumia mbegu zinazostahimili ukame na wananchi wote kutunza vipato vyao badala ya kuendekeza matumizi yasiyo ya lazima.

Mgeni maalum katika ibada hiyo, Mbunge wa Iringa Mjini, Jesca Msambatavangu, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Iringa, aliwahimiza waumini kuishi kwa mujibu wa maandiko matakatifu ili kukabiliana na changamoto za kidunia.

Alisema kila mtu anapochukua nafasi yake kikamilifu katika familia na jamii, matatizo mengi yanayowakabili vijana kama ukatili wa kijinsia na mmomonyoko wa maadili yanaweza kuepukwa.

Askofu Mstaafu wa KKKT Dayosisi ya Iringa, Prof. Owdenburg Mdegella, alizungumzia changamoto za kijamii zinazoukabili mkoa wa Iringa, zikiwamo matendo ya ukatili, udumavu na maambukizi ya UKIMWI.

Alisisitiza kuwa wazazi wana jukumu la kukemea na kuripoti vitendo vya ukatili dhidi ya watoto badala ya kuficha wahalifu.

# Mtoto adaiwa kuuawa wazazi wakiwa matembezini Krismasi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTOTO Grayson Kanyenye (6), anadaiwa kuuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani wakati mama yake akiwa matembezini usiku wa kuamkia Sikukuu ya Krismasi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, akizungumzia tukio hilo, alisema mwili wa mtoto huyo ulikutwa ndani ya nyumba ukiwa na majeraha shingoni.

Katabazi alisema tukio lilitokea majira ya saa 1:00 asubuhi katika Mtaa wa Bwawani, Ilazo Extension jijini Dodoma, nyumbani kwa Ofisa Uvuvi wa Mtera, Hamis Mohamed.

Alisema, Mohamed na mama wa mtoto huyo, walitoka kwenda matembezini na kumwacha chini ya usimamizi wa dereva bodaboda wa maeneo ya Ilazo Extension jijini hapa, aliyejulikana kwa jina la Kelvin Gilbert.

Kamanda Katabazi alisema bodaboda huyo walimfahamu kupitia huduma ya usafiri anayoitoa kwa familia hiyo.

"Bodaboda huyu aliachiwa mtoto ili amwangalie kipindi ambacho watakuwa kwenye matembezi wawili hao wakati wa usiku lakini waliporudi, mtoto hawakumuona hadi asubuhi majira ya saa 1:00 walipomkuta kwenye chumba akiwa ameuawa huku akiwa na alama za kupigwa na kitu kizito shingoni mwake," alisema.

Kamanda Katabazi alisema Jeshi la Polisi mkoani hapa linamshikilia bodaboda huyo kwa uchunguzi zaidi wa tukio hilo.

"Tumemkamata bodaboda huyo kwa ajili ya uchunguzi wa tukio hili. Yeye amekanusha kuhusika na jambo hili lakini tunaendelea na uchunguzi ili kubaini nini hasa kilitokea kwa mtoto huyu na kusababisha kifo chake," alisema Katabazi.

Aidha, Kamanda Katabazi alitoa wito kwa wazazi kuacha tabia ya kukabidhi watoto wao kwa watu ambao hawawajui vizuri ili kuepusha matukio kama hayo.

"Wazazi wanapaswa kuwa makini na watu wanaowaachia watoto wao kwa ajili ya kuwaangalia hawa walimwamini bodaboda na kumwachia mtoto wakati wao wanakwenda kutembea usiku lakini kilichotokea mtoto amepoteza maisha," alisema.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Mjumbe wa halmashauri kuu ya Chama Cha Mapinduzi wilaya ya Masasi mkoani Mtwara Shabani Saidi ambaye ni mchumi wa chama hicho mkoa wa Mtwara akizungumza na vijana wa umoja wa vijana UVCCM wilaya ya Masasi jana. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Atoroka kwa mumewe madai ya kunyanyaswa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MARIA Maladukwa (42) mkazi wa Kijiji cha Ghidika mkoani Manyara, ametoroka kijijini humo na kukimbilia mkoani Singida kwa madai ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia na mume wake.

Inadaiwa kuwa mume wake huyo alimfunga seng'enge na nondo ndogo katika miguu yake kama mtumwa kwa miezi miwili.

Mwanamke huyo ambaye amedhoofika mwili kutokana na mateso aliyodai kupewa na mume wake, alifika katika kijiji cha Matumbo, wilaya ya Singida huku akiwa na seng'enge katika mguu wa kushoto baada ya kutembea kwa saa 13 kutoka mkoani Manyara. Mwenyekiti wa kijiji cha Matumbo, Juma Maloda, akizungumza na gazeti hili jana, alisema walimpokea Maladukwa juzi katika ofisi za kijiji hicho saa 11:00 jioni.

Alisema baada ya kumpokea, walimpa chakula na kwenda kulala nyumbani kwa Mwenyekiti wa Kitongoji cha CCM, Abeid Ntandu.

Maloda alisema katika maelezo yake, mwanamke huyo alidai kuwa alifanikiwa kutoroka nyumbani kwake baada ya kukata seng'enge alizokuwa amefungwa katika mguu wa kulia na kubakia na za mguu wa kushoto.

Alisema mwanamke huyo ametembea kwa miguu kwa zaidi ya saa 13 akiwa na seng'enge na nondo ndogo vilivyobaki kwenye mguu wa kushoto kutoka mkoani Manyara hadi Singida kwa ajili ya kuwatafuta wazazi wake, ambao alidai wako eneo la Makurungu.

Mwanamke huyo alidai kuwa wakati akipatiwa mateso hayo, mume wake amekuwa akimwambia alimuoa ili aje apate utajiri wa magari na mifugo na kumlazimisha kushiriki kwenye vitendo vya uhalifu, vikiwamo wizi wa mahindi kwenye mashamba ya watu.

Kutokana na mateso hayo, ameomba msaada wa serikali kwa kuwa usalama wake uko hatarini iwapo mwanamume huyo ambaye amefahamika (majina tunayahifadhi kwa sasa) atapata taarifa za kuwapo kijijini hapo.

Mwenyekiti wa kijiji hicho alisema amekwisha wasiliana na polisi kuhusu tukio hilo na taratibu za kumsaidia zinafanywa na serikali.

Machi, mwaka huu, katika kikao cha kujadili vitendo vya ukatili wa kijijisia, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alisema matukio ya ukatili mkoani humo yamefikia 8,360 hadi Desemba, 2023.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Wafurahia faida nono mauzo ya korosho

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

WAKULIMA wa korosho wa Chama Kikuu cha Ushirika Masasi-Mtwara na Nanyumbu (MAMCU), kwa kauli moja wamekubali kuuza korosho tani 579 kwa bei ya juu ya Sh. 2,140 na bei ya chini ya Sh. 1,810.

Korosho hizo zimeuzwa mwishoni mwa wiki iliyopita katika mnada wa 11 wa korosho ulioendeshwa kwa mfumo wa soko la bidhaa Tanzania (TMX) katika kijiji cha Mpapura mkoani Mtwara na kuhudhuriwa na mamia ya wakulima wa zao hilo.

Wakizungumza baada ya kumalizika kwa mnada huo, viwanja vya Chama cha Msingi Mpapura ( AMCOS) wakulima hao walisema katika msimu huu zao hilo limekuwa na bei nzuri tofauti na misimu iliyopita.

Ally Mohamed, mkulima kijiji cha Mpupara, alisema bei za korosho zimeendelea kuwa za kuridhisha kwa wakulima tangu minada ya korosho ilipoanza Oktoba, mwaka huu.

Alisema kwa bei zilizoko sokoni zinazojitokeza kwenye minada kwa sasa, wanaendelea kuishukuru serikali kwa kuwa imewaheshimisha wakulima wa korosho hasa mikoa ya kusini.

Asha Juma ambaye pia ni mkulima, alisema kupitia bei hizo za korosho msimu huu, amepata fedha za kutosha baada ya kuuza zaidi ya tani sita na kwamba fedha hizo zimemsaidia kujenga nyumba ya kuishi na familia yake.

"Tunaipongeza serikali hasa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ametuheshimisha sisi wakulima kwa sababu bei ya korosho imekuwa ya kuridhisha msimu huu, tumepata maendeleo mazuri," alisema Juma.

Alisema kama serikali itaendelea kulinda thamani ya korosho, wakulima watakuwa na maendeleo makubwa ikilinganishwa na misimu ya miaka ya nyuma ambapo walikuwa wakilima na kutopata manufaa yoyote yale.

Fadhili Salumu, mkulima kijiji cha Libobe mkoani Mtwara, alisema wanafurahishwa na bei hizo, hivyo kupitia mnada wa 11 wanaridhia kuuza korosho zao tani 579 bei ya juu ya Sh. 2,140 na bei ya chini Sh. 1,860.

Mmwenyekiti wa MAMCU, Azam Julajula, alisema hadi sasa jumla ya minada 11 imefanyika na wakulima wamepata zaidi ya Sh. bilioni 365 za malipo ya minada 10 kati ya hiyo 11 ilifanywa ndani ya msimu huu wa korosho mwaka 2024/25

Alisema katika minada hiyo, zaidi ya tani 115,000 za korosho za chama hicho, zimeuzwa na wakulima kupokea malipo yao kwa wakati.

**HABARI KITAIFA**

# Othman awapoza ndugu waliofiwa na ndugu zao matukio tatanishi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka watu wa Shehia ya Kiungoni, Jimbo la Pandani Wilaya ya Wete Pemba, kuendelea kuwa na subira na umoja kutokana na vifo vya watu wawili vinavyodaiwa kuwa na utatanishi.

Amesema serikali italifuatilia kwa kina tukio hilo na kuhakikisha haki inatendeka kwa wahusika.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Habari cha Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman aliyasema hayo kwa nyakati tofauti katika vijiji vya Kiungoni Choni na Kimango alipofika kuzifariji familia za Amour Khamis (28) na Othman Hamad (75) wanaodaiwa kuuawa wakiwa mikononi mwa vyombo vya ulinzi.

Watu hao wanadaiwa kukamatwa Desemba 24, mwaka huu, majira ya usiku wakiwa majumbani mwao na siku iliyofuata maiti zao zilipelekwa katika Hospitali ya Chake Chake, Kusini Pemba.

Alisema tukio hilo limeendelea kuleta huzuni kubwa kwa watu wa Kiungoni na kutonesha majeraha ya matukio yanayofanana na yaliyotokea miaka iliyopita na hasa kwa kuzingatia watu hao walikamatwa kwa tuhuma na wamefariki dunia katika hali isiyotarajiwa.

Othman alisema kwa vile serikali jukumu lake la msingi ni kusimamia sheria pamoja na kuwalinda raia wake, inawajibika kufanya kila juhudi kwa waliohusika na tukio hilo hatimaye hatua za kisheria kuchukuliwa kwa vile hakuna mtu yeyote aliye juu ya sheria.

Alisema kumuua mtu mwenye tuhuma ni uhalifu sawa na mhalifu mwingine na kwamba mwenye kufanya jambo la kutoa roho ya mtu mwenye tuhuma anapaswa kuchukuliwa hatua sawa na mhalifu yeyote.

Mdogo wa marehemu Othman, Hamad, alimweleza Makamu wa Kwanza wa Rais kuwa kaka yake kabla ya kukamatwa usiku, mchana walikutana akiwa mzima wa afya na hakuwa na tatizo lolote la kiafya na kwamba wamepata mshtuko kutokana na taarifa za kuuawa kwake.

Alisema maiti za marehemu wote zilikuwa na hali inayofanana ya majeraha katika sehemu mbalimbali za miili yao ikionesha kupigwa vibaya na kuvuja damu sehemu mbalimbali, ikiwamo kichwani .

Salim ameacha watoto saba kati yao sita ni wanawake na mmoja mwanamume na kizuka mmoja wakati Amour waliyeuawa pamoja ni kijana ambaye alikuwa hajaoa.

# KKKT yazindua mradi kupambana na ukatili

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

KANISA la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) limezindua mradi wa "Pamoja Tuyajenge" ukiwa na lengo la kutoa elimu kwa watu wenye ulemavu na ukatili wa kijinsia kwa kuwa makundi hayo yanakabiliwa na matatizo ya unyanyapaa kwenye jamii.

Uzinduzi huo ulifanyika juzi katika Halmashauri ya Mji wa Makambako ambapo mradi huo upo chini ya Idara ya Vijana wa KKKT makao Makuu Arusha.

Wakizungumza baada ya uzinduzi huo, baadhi ya watu wenye ulemavu mjini Makambako, Rose Masegense, alisema licha ya jitahadi zinazofanyika ili kukabiliana na vitendo vya ukatili bado kuna tatizo la kutosikilizwa na baadhi ya taasisi binafsi na zile za serikali hasa pale wanapohitaji huduma.

"Ukienda kwenye ofisi za serikali kusikilizwa inakuwa shida na kwenye taasisi hizi binafsi utakapoingia mlemavu wakajua ni mlemavu wa aina fulani au umeshikiliwa wanakuwa na ile dhana umekwenda kuomba, hivyo tunaomba waondokane na hiyo dhana mbaya," alisema.

> **"Ukienda kwenye ofisi za serikali kusikilizwa inakuwa shida na kwenye taasisi hizi binafsi utakapoingia mlemavu wakajua ni mlemavu wa aina fulani au umeshikiliwa wanakuwa na ile dhana...**

Magdalena Kinyunyu alisema bado kuna baadhi yao wanafungiwa ndani hali inayosababisha wakose haki zao, huku wakiomba kuwezeshwa mitaji itakayowasaidia kuanzisha miradi ya kiuchumi na kuachana na tabia ya kuwa omba omba.

Ofisa Ustawi Jamii Halmashauri ya Mji wa Makambako, Maria Mkude, alisema bado kuna vitendo vya ukatili kwa watu wenye ulemavu, huku wakitaka jamii kuacha tabia ya kuwafungia ndani watoto wenye ulemavu na kuripoti kwenye mamlaka husika wanapokutana na matukio hayo.

Mmoja wa viongozi wa kidini, Shekhe Ibrahaim Chang'a, alisema jamii inapaswa kushirikiana ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanaishi katika mazingira rafiki ambayo yanawawezesha kupata mahitaji yote ya msingi bila kutengwa.

Mchungaji wa Kanisa la Moravian, Ezekiah Mwashibanda, aliitaka jamii kutowabagua watu wenye ulemavu ili kupata haki zao.

Awali, akitambulisha mradi huo, Mwenyekiti wa Vijana wa KKKT, Anania Ndondole, alisema wameanzisha kampeni hiyo ambayo itatekelezwa kwa mwaka mmoja kutokana na watu wenye ulemavu kufanyiwa ukatili wa kunyanyapaliwa hata kuzuiliwa kuhudhuria kwenye nyumba za ibada.

"Watu wenye ulemavu ni moja ya kundi ambalo halijapewa kipaumbele cha kutosha katika masuala mengi, iwe katika masuala ya uongozi, iwe katika masuala mbalimbali ya kijamii lakini ndilo kundi ambalo limeathirika na vitendo vya ukatili wa kijinsia," alisema Ndondole.

Ofisa Tarafa ya Makambako Wilaya ya Njombe, Frola Nyato, aliwataka wadau kushirikiana na serikali hasa kuwaibua watu wenye ulemavu ambao bado hawajafikiwa na kuhakikisha wanapelekwa shule.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA IRINGA, MBEYA NA DODOMA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Dodoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa tarehe 27 Desemba, 2024 hadi 02 Januari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Ijumaa tarehe 27 Desemba, 2024 hadi Alhamisi tarehe 02 Januari, 2025.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**
1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**
- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 8 na kubonyeza, baada ya hapo atachagua namba 2 na kubonyeza, Kisha atachagua Namba 3 (Tume Huru ya Uchaguzi) na hapo, atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

**Limetolewa tarehe 19 Desemba, 2024 na:**

**Saida Hilal Mohammed**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

218302902



**NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND**

**Tender No. TR187/2024/2025/G/KFW/01**
**For**
**Supply, Installation and Commissioning of the Enterprise Routers and Firewalls**

**Invitation for Tenders**

**Date: 27/12/2024**

1. The National Health Insurance Fund has received grant from the KFW towards the cost of Supply, Installation and Commissioning of Enterprise Routers and Firewalls, and it intends to apply part of the proceeds of this grant to cover eligible payments under the contract for Supply, Installation and Commissioning of Enterprise Routers and Firewalls.
2. The National Health Insurance Fund now invites sealed tenders from eligible Suppliers of Supply, Installation and Commissioning of Enterprise Routers and Firewalls.
3. Tendering will be conducted through the National Competitive tendering procedures specified in the Public Procurement Regulations, 2024 – Government Notice No. 518, and is open to all Tenderers as defined in the Regulations.
4. Interested eligible Tenders may obtain further information from and inspect the Tendering Documents at the office of the Secretary of the Tender Board, National Health Insurance Fund, and P. O. Box 1437 Dodoma – Tanzania from 08:00 to 16:00 or through e-mail (**group.pum@nhif.or.tz**) on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays.
5. A complete set of Tendering Document(s) in English and additional sets may be purchased by interested Tenderers on the submission of a written application to the address given under paragraph 4 above and upon payment of a non-refundable fee of Hundred thousand only Tanzania shillings (TZS. 100,000/=). Payment should be made through a control number upon submission of written application.
6. All Tenders must be accompanied by a Tender Security in an acceptable form in the amount of 10% of the tendered price.
7. All tenders in one original plus two copies, properly filled in, and enclosed in plain envelopes must be delivered to the address; Office of the Secretary of Tender Board, Second floor, NHIF-HQ Building in Dodoma-Tanzania at or before 17th January 2025 at 10:00 Hours. Tenders will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Tenderers' representatives who choose to attend in the opening at the NHIF-HQ Board room, second floor , NHIF building Dodoma –Tanzania.
8. Late Tenders, Portion of Tenders, Electronic Tenders, Tenders not received, Tenders not opened and not read out in public at the tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**ACCOUNTING OFFICER**
**NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND**
**P. O. BOX 1437, DODOMA, TANZANIA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matukio kuhusu ukatili yamalizwe kwa vitendo

**VITENDO** vya ukatili vimekuwa vikishamiri siku hadi siku katika jamii huku jitihada za kutokomeza zikiwa zinaendelea. Vitendo hivyo, kila uchao vimekuwa vikisikika na kuripotiwa kwenye vyombo vya habari nchini.

Miongoni mwa vitendo hivyo, ni mauaji baina ya wanandoa yanayosababishwa na wivu wa kimapenzi, msongo wa mawazo na mmomonyoko wa maadili huku kwa sehemu kubwa, wanaume wakionekana ndio wahusika wakubwa kwa kuwaua wake zao na watoto pia. Wako wengine ambao wameripotiwa kuwanyonga, kuwachinja wenza wao kisha kuwafukia.

Yako pia baadhi ya matendo yaliyoripotiwa kwa baadhi ya kinababa kudaiwa kuwaua wake na watoto wao kwa madai vipimo vya vinasaba kuonesha kuwa si watoto wao. Iko pia taarifa iliyoripotiwa kuwa mume alimuua mke wake baada ya kukuta amepikiwa nyama wakati aliacha fedha kwa ajili ya maharage na mboga ya majani? Kwa kukuta chakula hicho, mawazo yalimfikirisha kwamba amepewa na mwanamume wake wa pembeni!

Kwa ujumla, matukio hayo yanazidi kuwa tishio katika jamii licha ya wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikali, wa dini, wanaharakati na vyombo vya habari kukemea siku kwa siku. Machi, mwaka huu, kwa mfano, katika kikao cha kujadili vitendo vya ukatili wa kijinsia, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alisema matukio ya ukatili mkoani humo yamefikia 8,360 hadi Desemba, 2023.

Takwimu hizo zinaonesha kwamba matukio hayo yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku jambo ambalo linaonensha kwamba watu sasa hawana hofu ya Mungu. Wanadiriki kuwafanyia unyama binadamu wenzao bila huruma na hata kuwasababishia vifo na ulemavu wa kudumu.

Hali hiyo pia imewafanya binadamu kuwa zaidi ya hayawani na kuondoa uhalisia kwamba waliumbwa kwa mfano wa Mungu, hivyo wanapaswa kutenda mambo mengi yakiwamo matendo ya huruma.

Moja ya matukio yaliyoripotiwa katika gazeti hili ni mwanamke mmoja, aliyejulikana kwa jina la Maria Maladukwa (42) mkazi wa kijiji cha Ghidika mkoani Manyara, kutoroka nyumbani kwake na kukimbilia mkoani Singida kwa madai ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia na mume wake.

Kwa mujibu wa habari hiyo, inadaiwa kuwa mume wake huyo alimfunga seng'enge na nondo ndogo katika miguu yake kama mtumwa kwa miezi miwili, hivyo kumsababishia maumivu na kudhoofika mwili kutokana na mateso aliyodai kupewa na mwenza wake huyo. Kutokana na mateso hayo, mwanamke huyo alifika katika Kijiji cha Matumbo, wilaya ya Singida huku akiwa na seng'enge katika mguu wa kushoto baada ya kutembea kwa saa 13 kutoka mkoani Manyara.


Kwa mujibu wa uongozi wa Kijiji hicho uliompokea mwanamke huyo, alidai kuwa alifanikiwa kutoroka nyumbani kwake baada ya kukata seng'enge alizokuwa amefungwa katika mguu wa kulia na kubakia na za mguu wa kushoto na alikimbia kwa nia ya kuwatafuta wazazi wake na kuomba hifadhi.

Kwa jumla, matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto yamekuwa sawa na wimbo usio na mwisho katika masikio ya wanadamu kutokana na ukweli kwamba kila siku yamekuwa yakisikika.

Kutokana na ukweli huo, ni vyema sasa kila mwanajamii akasimama kwa nafasi yake kukemea vitendo hivyo ambavyo vinaiweka jamii ya Kitanzania katika taswira hasi na kuonekana kama ni mambo ya kawaida. Ni dhahiri kwamba kama vitendo hivyo vitaachiwa na kuendelea kushamiri, kuna athari kubwa za kijamii na kiuchumi ndani ya nchi.

Kama ule msemo wa mapambano dhidi ya Ukimwi unavyosema 'It Begins With You' kwa maana kwamba mapambano yanaanza na wewe, ni vyema sasa kila Mtanzania akafahamu kwamba mapambano dhidi ya ukatili yanaanzia kwake. Tanzania bila ukatili inawezekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Tuntule Swebe

# Hii biashara ya kukabana na kupora simu tukisherehekea, tujitafakari !

**KIPINDI** cha msimu wa Krismasi na Mwaka Mpya, imekuwa kawaida ya vijana kuunda mikusanyiko isiyo na manufaa.

Staili zao huwa wanatengeneza magenge ya uhalifu, wakiamini kupitia mikusanyiko hiyo itazaa matunda kiuchumi kwao.

Dhana yao kuu, wanafikiri kwamba watu kwa nyakati hizo wanakuwa na 'chochote kitu' kwa sababu wamejikusanyia kipato kwa matumizi ya sikukuu hizo.

Hilo linatolewa ufafanuzi na kijana Salehe Hassan, mkazi wa Mbezi Matosa wilayani Ubungo, Dar-es Salaam, anayesema nyakati za sikukuu, kumekuwapo matukio ya uporaji wa simu na hasa kwa wanawake wanaotoka kuwatembelea ndugu zao.

Anatamka kwamba, vibaka na wahuni hutumia mazingira hayo kufanya uhalifu tajwa.

Kwa mujibu wa Salehe, cha msingi kinachotakiwa kuwapo ni ulinzi shirikishi nyakati za usiku na mahali penye ukabaji. Kunatajwa suala la kukabwa, kukabana linatakiwa kushughulikiwa kwa nguvu za kisheria kabla ya hazijavuka mbali.

Hapo kijana huyo wa Mbezi ananena lake, akiwataka wahusika hao waache kufanya hivyo, maana ina wapelekea katika hatua zingine, wapo wanaochukua hatua za mkononi, falsafa zao zikiwaambia wako sahihi .

Vilevile, mkazi mwingine anayejitambulisha kwa jina, Joseph Pascal , ni kwamba nyakati za sikukuu wanakumbana na mikasa kama hiyo, akitaja maeneo mengine kama Mwananyamala, wilayani Kinondoni, kuna mambo ya aina hiyo.

Anasema, kuna watu wengine wanaojishughulisha na wizi, kama sehemu ya kutimiza wajibu wa kiuzazi katika familia yao na ili kupata chakula bora.

Msemaji huyo anataja watu hao inawalazimu waingie mtaani na kufanya 'ukwapuzi', jambo linaloweka maisha yao hatarini, kwani wanakuwa jirani na kifo ama kwa kipigo au kutiwa nguvuni kwenye vyombo vya serikali.

Hivyo ni muhimu watu kujipa majukumu sahihi na wanayoyaweza na wasiyoyaweza waachane nayo.

Jeshi la Polisi nchini, nalo linasema kuwa hali ya usalama wa nchini iko shwari, huku likibainisha kuwapo uhalifu mkubwa na mdogo unaoendelea kudhibitiwa kupitia mikakati mbalimbali iliyobuniwa.

Hiyo inatajwa kuendelea kutekelezwa kwa kushirikisha wananchi na wadau wengine wanaozuia uhalifu wa kijinai nchini. Akitoa taarifa yake, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, SACP David Misime, anasema katika kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka, jeshi hilo linaorodhesha mikakati ya kuhakikisha wanaendelea kuelimisha na kuzuia uhalifu, kufanya misako na operesheni kuwakamata wavunja sheria.

SACP Misime anasema kuwa polisi inawatahadharisha wazazi na walezi katika sikukuu hizo za mwisho wa mwaka, kutokuwaruhusu watoto kwenda kwenye maeneo ya mikusanyiko bila uangalizi sahihi.

Polisi nchini inasema, hali ya usalama wa nchi ni shwari, huku likibainisha kuwa uhalifu mkubwa na mdogo unaendelea kudhibitiwa kupitia mikakati iliyobuniwa na kuendelea kutekelezwa kwa kushirikisha wananchi na wadau wengine katika kuzuia uhalifu wa kijinai hapa nchini.

Anashauri hali ya kuwapo busara kwa kila mtu kutambua nyakati za sikukuu ni za upendo na ushirikiano kwa kila mmoja.

Hivyo, anataja ni vyema watu kukubaliana na hali zao na siyo kujipa majukumu asiyoyaweza au yasiyopendeza akitoa mfano wa kumdhuru mwingine, kutaka kupata chochote, kwani huwa na mwisho mbaya.

**HABARI KITAIFA**

# Jela miaka 30 kwa kubaka mwanafunzi

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKULIMA na mkazi wa Kijiji cha Nkowe, Ruangwa mkoani Lindi, Abdallah Hassan (30), amehukumiwa kifungo cha miaka (30) jela baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka mwanafunzi wa umri wa miaka 10.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Kamishna msaidizi (ACP) John Imori, alisema hayo jana ofisini kwake alipokuwa anatoa taarifa ya utendaji kazi na mafanikio yaliyopatikana kipindi cha Desemba, mwaka huu.

Alisema mshitakiwa alikamatwa kijijini hapo Februari 09, mwaka huu, akiwa anatekeleza unyama huo na kufikishwa kituo cha polisi na kukiri kufanya kosa hilo alipokuwa akihojiwa na askari wakati anachukuliwa maelezo ya awali.

Imori alisema ilipofika Februari 29, baada ya upelelezi kukamilika, mtuhumiwa akafikishwa mahakamani kusomewa shtaka lililomkabili.

Kwa mujibu wa Kamanda Imori, baada ya kumkuta anayo hatia ya kufanya unyama huo, Desemba 24, mwaka huu, Mahakama ya Wilaya ya Ruangwa ikamhukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 jela.

"Hivi ninapozungumza na nyinyi hapa leo na nyinyi waandishi, tayari mshitakiwa yuko gerezani akitumikia adhabu yake," alisema.

Kamanda Imori alisema katika kipindi cha Desemba, jeshi la Polisi wamefanikiwa mambo mbalimbali ikiwamo kupunguza vitendo vya wizi na uhalifu ndani ya mkoa Lindi, ikiwa ni pamoja na kukamata pikipiki aina ya HAOJUE MC 559 EAL iliyokuwa imeibwa Kijiji cha Mtama na kuikamata Newala mkoani Mtwara Desemba 24, mwaka huu.

Kamanda huyo aliendelea kutoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Lindi kuwa makini ikiwamo kuchukua tahadhari ya kuchunga watoto na kuangalia usalama wa nyumba zao wakati wa kusheherekea mwaka mpya wa 2025.

"Sikukuu ya mwisho wa mwaka kwa kawaida inakuwa na mambo mengi ikiwamo wizi, hivyo nawaomba wananchi wachukue tahadhari kwa watoto na nyumba zao kutoziacha peke yao," alisema.

Pia Kamanda Imori alisema Jeshi la Polisi kupitia askari wake wamejipanga kuhakikisha mkoa wa Lindi unakuwa salama kwa nyakati zote na zile za sikukuu, ikiwamo kutoruhusu wananchi kuchoma moto matairi barabarani, kuondoa usumbufu kwa waendesha vyombo vya moto na watembea kwa miguu.

# Wananchi 100,000 kunufaika mradi wa maji mjini Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

ZAIDI ya wananchi 100, 000 wanatarajia kunufaika na mradi wa maji wa miji 28 katika kata tatu za Halmashauri ya Mji wa Njombe ambazo ni Mji Mwema, Njombe Mjini na Ramadhani.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Njombe, (NJUWASA), Robert Lupoja, aliyasema hayo juzi katika eneo la mradi la ujenzi wa matangi katika Mtaa wa Lunyanywi.

Lupoja alisema mradi huo unajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 40 na unatarajia kuwaondolea adha wananchi kuhusu upatikanaji wa maji safi na salama.

Alisema kata hizo zinawakazi wapatao 91, 000 na mahitaji yao ya maji kwa siku ni lita milioni 10 lakini NJUWASA inazalisha lita milioni tano kwa siku, hivyo kuna upungufu wa maji lita milioni tano hali inayosababisha kuwepo kwa mgawo wa maji wa siku mbili hadi tatu kwa baadhi ya maeneo.

Alifafanua kuwa mradi huo ukikamilika utaongeza kiwango cha maji hadi lita milioni 17 kwa siku hali itakayosaidia kuongeza uwezo kwa Njuwasa kutoa huduma kwa muda wa saa 24 kwa siku zote kwa juma.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alisema mradi huo utahudumia Halmashauri ya Mji wa Makambako na Njombe ambapo ameridhishwa na hali ya utekelezaji wa mradi huo na kumtaka mkandarasi kuongeza kasi ya utekelezaji kwa kufanya kazi kwa sehemu zote tatu. "Nakuomba mkandarasi utoe fursa za kupata zabuni za bidhaa za ujenzi ili wazawa waweze kunufaika na fedha za mradi huu na kuongeza mzunguko wa fedha Mjini Njombe na kuona manufaa ya uwepo mradi huu katika wilaya yetu," alisema.

# DC asikitishwa watoto kudondoka shuleni

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Wang'ing'ombe mkoani Njombe, Zakaria Mwansasu, amesikitishwa na vitendo vya wanafunzi kudondoka mara kwa mara wakiwa shuleni huku vipimo vikishindwa kuonesha ugonjwa unaowakabili.

Alisema hayo juzi wakati akizungumza na wenyeviti wa vijiji pamoja na mitaa wakati wa semina elekezi kwa wenyeviti hao baada ya uchaguzi.

Alisema katika Shule ya Msingi Uhenga pamoja na Uhekule zilizopo wilayani humo wanafunzi wamekuwa wakidondoka na vipimo vikishindwa kuonesha ugonjwa wao.

"Shule ya Msingi Uhekule watoto wanadondoka, tumejitahidi kuwachukua na kuwapima lakini wale watoto hawaumwi chochote na baada ya kufuatilia kwa kina tukabaini sababu ni kwamba uliokuwa msitu wa kijiji umefyekwa na ndio ulikuwa msitu wa tambiko sasa hii ni imani lakini watoto wanadondoka" alisema Mwansasu.

Mwansasu alisema katika vijiji kuna wazee wenye mila na tamauni zao zisizovunja sheria, hivyo wanao wajibu wa kuwasikiliza ili kuepuka changamoto pamoja na kwenda kusimamia kwa kuyatunza na kuhuisha misitu iliyopo vijijini.

"Tunao wazee katika vijiji vyetu ambao wana mila na tamaduni zao lakini hizi mila na tamaduni zao hazivunji sheria wakikwambia hili pori siyo la kuuza wala siyo la kukata kuni liache, wakikwambia huu mti hapa siyo wa kuutoa uache" aliongeza Mwansasu.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**TAARIFA KWA UMMA**

**MAOMBI YA LESENI CHINI YA MFUMO WA LESENI KUTANIKO**

Taarifa inatolewa kwa Umma kwamba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imepokea maombi ya leseni chini ya mfumo wa leseni kutaniko kutoka kwa waombaji wafuatao: -

| Na. | JINA LA MUOMBAJI | AINA YA LESENI | WANAHISA/URAIA | HISA % |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Barmedas.Com Limited | Leseni ya Kiwilaya ya Huduma ya Mifumo Tumizi bila Miundombinu ya Mawasiliano | i. Hiroy N. Barmeda - Mtanzania | 70 |
| | | | ii. Hiteshi H. Barmeda - Mtanzania | 30 |
| 2. | Wakapay Fintech Company Limited | Leseni ya Kitaifa ya Huduma ya Mifumo Tumizi bila Miundombinu ya Mawasiliano | i. Mutina Group GMBH - Mswiss | 49 |
| | | | ii. Calvin Sylivestre Mitti - Mtanzania | 15 |
| | | | iii. George Mtemahanji - Mtanzania | 36 |

Kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta, Sura 306 ya sheria za Tanzania, maoni ya kimaandishi yanakaribishwa kutoka kwa yeyote kuhusiana na utoaji wa leseni kwa waombaji yafike TCRA ndani ya siku kumi na nne (14) tangu siku ya kutoka tangazo hili. Maoni yatakayopokelewa yatazingatiwa na TCRA itakapokuwa inayafanyia kazi ombi hili.

**Maoni yatumwe kwa:**
Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,
S.L.P 474 | 14414 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 241 2011-2
Nukushi: +255 22 2412009
Barua pepe: dg@tcra.go.tz

Imetolewa Tarehe **27 Desemba, 2024.**

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz

# Wajasiriamali wafundwa nidhamu ya fedha

**Na Mwandishi Wetu**

WAJASIRIAMALI katika Manispaa ya Sumbawanga wametakiwa kuwa na nidhamu ya fedha na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa ili kunufaika na mikopo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Sumbawanga, Gabriel Masinga, alitoa ushauri huo wakati wa kutoa mafunzo kwa wajasiriamali ya namna ya kutumia fedha watakazo kopa.

Alisema wajasiriamali wamepewa kanuni za kwenda kufanya uzalishaji wenye tija kwa bidii ili wairudishe na wengine kukopa tena.

Akifungua mafunzo hayo, Masinga aliwahimiza wanufaika hao kwenda kufanya uzalishaji wa fedha na kuongeza kipato kwa kasi, ikiwa ni pamoja na ubunifu katika biashara ili kupata matokeo chanya kwa maendeleo endelevu ya uchumi na biashara zao.

Pia aliwataka wanufaika hao kuwa na nidhamu ya fedha na kuachana na matumizi holela ya anasa ili kuinua uchumi binafsi, hatua itakayoleta maendeleo makubwa ya jamii.

Kikundi cha Mshikamano Kanondo na Annointed Group ni miongoni mwa vikundi 14 vilivyopatiwa mafunzo na ni wanufaika wa mkopo huo katika Manispaa ya Sumbawanga.

Waliishukuru serikali kwa kutenga fedha za mkopo kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu na kuahidi kuzingatia elimu ya fedha waliyopatiwa.

Katika hatua nyingine, Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Sumbawanga, Frank Mateni amesema vikundi 14 vimepewa mkopo wa milioni Sh. 223 ili kwenda kujiinua kiuchumi.

Mateni alisema vikundi vya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu waliyoomba mikopo ndani ya muda wa dirisha la mikopo na vinavyotarajiwa kupatiwa mikopo hiyo ya asilimia kumi kwa robo ya pili ya Oktoba hadi Desemba ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Alisema vikundi tisa vya wanawake, vikundi vinne vya vijana na kikundi kimoja cha watu wenye ulemavu wamenufaika na mkopo huo.

Tangu kufutwa kwa huduma ya mikopo kutolewa kwa halmashauri zote nchini Mkoa wa Rukwa umeanza na dirisha la mikopo kwa robo ya pili.

**Pia aliwataka wanufaika hao kuwa na nidhamu ya fedha na kuachana na matumizi holela ya anasa ili kuinua uchumi binafsi, hatua itakayoleta maendeleo makubwa ya jamii.**



Maofisa kutoka Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ambao wameweka kambi katika pori la Doroto wilayani Manyoni mkoani Singida wakitoa mafunzo kwa wananchi wa vijiji vinavyopata adha ya tembo namna ya kukabiliana na wanyama waharibifu kwa kutega mizinga ya nyuki kwenye mapito ya tembo, juzi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wataka jinsia kuzingatiwa mafunzo ya kilimo

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WADAU wa kilimo wameagizwa kuzingatia jinsia wakati wakitoa mafunzo mbalimbali hasa ya kilimo ili kuwafanya wawanake kupata ushiriki na elimu ya kile wanachofanya kutokana na wingi wao katika maeneo mbalimbali ikiwamo mashambani.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Musa Ally, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya wakulima wa mpunga kutoka wilaya za Iringa mkoani Iringa, Ulanga na Malinyi mkoani Morogoro juu ya kuwajengea uwezo wa namna ya kutumia teknolojia za kisasa katika kuboresha kilimo cha mpunga kwa kuzingatia mnyororo wa thamani yaliyofadhiliwa na Shirika la Chakula la Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kwa msaada kutoka Korea Kusini yaliyofanyika mjini hapa.

Dk. Musa alisema utoaji wa mafunzo kwa kuzingatia jinsia ni muhimu kutokana na kuwa zaidi ya nusu ya Watanzania ni wanawake ambao ndio wanaoingia shambani kulinganisha na wanaume ambao wengi huonekana kwenye mafunzo huku wakiwa hawaingii shambani.

Aidha, Dk. Musa aliiagiza Taasisi za Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa kushirikiana na FAO Tanzania kuhakikisha wanatoa elimu ya matumizi ya zana bora za kilimo cha mpunga ili kuongeza uzalishaji wa mpunga.

Pia alisgizas taasisi hizo zisimamie suala la upatikanaji kwa masoko ya uhakika wa mazao hayo. Dk. Musa alisema wakulima wengi kilio chao kikubwa ni masoko, hivyo wakati wanapewa na elimu ya kilimo cha mpunga, wapewe na elimu ya masoko hali itakayowasaidia kuongeza uzalishaji huku wakiwa na uhakika wa masoko.

"Ikiwa suala la uhakika wa masoko halitawekwa wazi kuwa wapite njia zipi kuyafikia, juhudi za uzalishaji wa mpunga zinaweza kupungua kutokana na asimilia kubwa ya wakulima walíopo kwa sasa hukosa masoko na kubakiwa na mpunga mwingi. Pengine hali hiyo inaweza kutishia juhudi za wizara katika kuhakikisha kilimo hicho kinakua nchini" alisema.

Awali, Mkurugenzi wa Uhaulishaji wa Teknollojia na Uhusiano kutoka TARI, Dk. Sophia Kashenge, aliwataka vijana kutambua kuwa kilimo ni sekta inayokua kwa asilimia 4.2 kwa sasa, ukuaji amba oni mdogo na kwamba kilimo kinapaswa kukua kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 ili kuchangia ongezeko la uzalishaji na kuwa na uhakika wa chakula.

Alisema Tanzania inaongezeka watu kila kukicha, hivyo wasipokuwa makini ongezeko la watu litazidi la chakula, hivyo kuingia kwenye mtihani au vurugu kwa sababu wanasema mtu mwenye njaa hatawaliki.

Dk. Kashenge alisema ongezeko la watu Tanzania linakua kwa asilimia 3.2 ambalo ni kubwa sana kwa Afrka na duniani wakati kiwango cha Afrika ni asilimia 2.0 na Duniani ni asilimia moja.

Alisema hali hiyo inaonesha kasi ya kuzaliana Tanzania kuwa kubwa na kwamba ni lazima mikakati yote ilenge kuhimiza kilimo ili kuwa na uhakikika wa chakula.

Hata hivyo, Dk. Kashenge alisema uzalishaji wa chakula nchini uko vizuri na mahitaji ya chakula ni tani milioni 16 na uzalishaji ni tani milioni 20, hivyo kuna ziada ya tani milioni 4.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkazi wa FAO-Tanzania, Nyabenyi Tipo, Mwakilishi wa FAO-Tanzania, Dk. Diomedes Kalisa, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha wakulima wa Tanzania wanakuwa na uzalishaji shindani.

Alisema kwa sasa Tanzania inashika nafasi ya kwanza kwa Afrika Mashariki na kwa Afrika imeshika nafasi ya tatu ikitanguliwa na nchi ya Nigeria katika kuzalisha mpunga.

# Wanufaika wenye ulemavu TASAF waishukuru Serikali

**Na Faustine Feliciane**

WANUFAIKA wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambao ni watu wenye ulemavu wameomba msaada serikalini, huku wakisema mfuko huo umekuwa msaada na kubadilisha maisha yao.

Hivyo, wamemuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuuongezea uwezo mfuko huo ili kuwafikia watu wengi zaidi.

Akizungumza wilayani Kibaha mkoani Pwani, mmoja wa wanufaika hao ambaye ni mwenye ulemavu, Amina Mrupe, alisema awali walikuwa wakipitia changamoto kubwa kutokana na hali zao, lakini uwepo wa ruzuku hiyo ya TASAF imewabadilishia maisha yao.

"Tunamuomba Rais Samia kuiongezea nguvu TASAF ili kuwafikia watu wengi zaidi, tuna uhitaji mkubwa kutokana na hali zetu hivyo tunaendelea kuiomba serikali kuendelea kutusaidia," alisema Amina.

Alisema kupitia TASAF wameweza kuanzisha biashara mbalimbali kama vile kuuza karanga, kutengeneza batiki, viungo vya chai, chakula pamoja na sabuni na kupitia biashara hizo wamekuwa wakipata fedha kujikimu kimaisha.

Alisema mbali ya kupewa ruzuku hiyo ya kila mwezi ambayo walikuwa wanapatiwa kila baada ya miezi miwili pia amepewa mtaji wa Sh.500,000 ambazo zimemuwezesha kuanzisha biashara ya batiki pamoja na kuuza karanga.

"Maisha yamebadilika siyo kama zamani, sasa hivi napata mahitaji yangu muhimu mimi na familia yangu, ndiyo maana tunaiomba serikali kutuangalia kwa karibu watu wenye ulemavu lakini pia kuiongezea nguvu TASAF, kwa kweli inatusaidia sana," alisema.

Mnufaika mwingine, Nuru Ally mkazi wa Kigogo jijini Dar es Salaam ambaye ni mlemavu wa kutoona alisema kwa sasa ameondolewa kwenye orodha ya wanufaika wa mfuko huo baada ya hali yake ya kiuchumi kuimarika.

Alisema kuwa kupitia TASAF ameweza kuwa na ujuzi wa anatengeneza viungo vya chai, viungo vya chakula na sabuni ya chooni na hivyo kuendesha maisha yake.

Walemavu, alisema wamekuwa wakionekana kama wanapenda kuwa ombaomba lakini kupitia TASAF amekuwa akifanya shughuli zinazomuingizia kipato na kuweza kuhudumia familia yake akiwa na watoto wanne.

Hata hivyo wanufaika hao wamesema changamoto kubwa waliyonayo ni soko la kuuza bidhaa wanazozizalisha.



# Askofu ataka maombi kukabili ajali

**Na Steven William,** MUHEZA

ASKOFU wa Dayosisi ya Kaskazini Mashariki ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Msafiri Mbilu, amewahimiza wakristo kumpigia magoti Mungu ili 'zimwi' la ajali za barabarani zinazolitesa taifa kwa sasa likome kwa kuwa zinakatisha maisha ya watu wengi.

Dk. Mbilu alisema idadi kubwa ya Watanzania na wageni wanaopata ajali hizo, wengine wanapoteza maisha na wengine kupata ulemavu wa kudumu katika kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Ujumbe huo wa Askofu, uliosomwa jana katika Usharika wa Muheza Mjini na Katibu Mkuu wa Dayosisi hiyo, Julius Madiga, unasema ongezeko la ajali linatishia mustakabali wa taifa kwa sasa.

Alisema kutokana na mwenendo huo, iko haja sasa Watanzania kwa umoja wao, kupiga goti na wengine kuomba dua ili Mwenyezi Mungu, aliepushe taifa na zimwi la ajali linaloandama kila kona ya nchi.

**"Tuko hapa Arusha kwa siku tatu nne kwa mkutano, kwa namna yeyote na sisi tushiriki kutatua au kupunguza baadhi ya changamoto...**

"Kwa niaba ya Baba Askofu Mbilu, naomba Mungu alete amani na kama taifa atuepushe na majanga yanayotokea hivi sasa ya ajali za barabarani.

Vilevile, atuepushe na yote yanayoleta uvunjifu wa amani ya nchi, majanga mbalimbali na mikosi," alisema.

Mchungaji Kiongozi wa KKKT Usharika wa Muheza Mjini, Elias Majo, aliwaagiza waumini wa kanisa hilo kuendelea kuliombea taifa ili mwaka ujao uwe mwaka wa amani,upendo na mshikamano kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Katika hatua nyingine, Paroko wa Parokia ya Kristo Mfufuka iliyoko Muheza, Padri Martine Kihiyo, aliwakumbusha waumini wa kanisa hilo kutenda mema ya kumpendeza Mungu, upendo na mshikamano kuingia Mwaka mpya wa 2025.

Mchungaji wa Kanisa la Anglikana, Mtaa wa Madaba, Paul Luhinga, alisema kuwa anamshukuru Mungu kuiona Sikukuu ya Krismasi, huku akiwaomba waumini kuendelea kumcha Mungu na kutenda mema duniani.



Mkurugenzi wa Shirika la Madini la Taifa (Stamico) Dk Venance Mwasse (kulia) akizungumza na Mkurugenzi wa kampuni ya Franone Mining Ltd inayochimba madini ya Tanzanite kitalu C na D mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mradi wa kupunguza uwindaji haramu sasa waanza kuleta matokeo chanya

**Na Godfrey Mushi,** LONGIDO

SHIRIKA la World Wildlife Fund (WWF), limeanza kupata matokeo chanya katika mkakati wake wa kupunguza uwindaji haramu wa wanyamapori na kunusuru uharibifu wa mazingira.

Hatua hiyo ni baada ya kuhamasisha wafugaji wa jamii ya Kimasai katika Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, kujikita zaidi kwenye uzalishaji wa alizeti.

WWF inatoa elimu kwa jamii hiyo ya Kimasai kuhusu kilimo mbadala cha alizeti, kandokando ya maeneo yanayopakana na shoroba.

Meneja Mradi wa Land for Life, unaotekelezwa na WWF katika Wilaya hiyo, Reguli Marandu, akizungumzia mkakati huo katika mahojiano maalum, alisema lengo la uhamasishaji wanaoufanya ni kuzuia ukataji miti ovyo, kuchoma mkaa, ujangili na uwindaji haramu wa wanyamapori.

Alisema kwa kipindi kifupi jamii imebadili maisha yao kiuchumi tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Shirika hilo linachochea mabadiliko ya kiuchumi kwa jamii ya Kimasai, wakati ambapo Soko la Eneo Huru la Afrika (AfCFTA) likiwa limefunguka, likikadiriwa kuwa na walaji zaidi ya bilioni 1.3 kutoka nchi 53 Barani Afrika.

"Wakulima katika Kijiji cha Engarenaibori, Kata ya Mairowa, wanalima sana alizeti kwa sababu ni miongoni mwa mazao ambayo hayashambuliwi na wanyamapori kama tembo. Dhana ya WWF tunataka jamii zile zinazoishi kwenye hayo mazingira pamoja na wanyamapori na mazingira yetu, vyote viwe vina ustawi ambao ni mzuri.

"Kwa hiyo ni vizuri wakulima wengine na wafanyabiashara ya mafuta ya kula hasa yanayotokana na alizeti, wakajifunza na kujipanga kuhudumia masoko makubwa ya ndani, kikanda na kimataifa ili kutengeneza mabilionea wa zao hilo," alisema.

Mmoja wa wakulima wa zao hilo aliyejengewa uwezo na WWF, Alex Sanka, mkazi wa Mairowa, alisema ameamua kulima alizeti kwa sababu lita moja ya alizeti anauza hivi sasa kwa Sh. 7,000 ikiwa haijafika sokoni.

"Mimi hivi sasa navuna alizeti kila baada ya miezi mitatu. Unajua huku maeneo ya pembezoni kuna wanyamapori wengi wakali na wanakulama mazao yetu, lakini hawali alizeti. Ni zao lisilokuwa na usumbufu ukiacha kushambuliwa na ndege.

"Mwanzo tulikuwa tukipata mazao hafifu, hasa maharage na mahindi ambayo yalikuwa yakishambuliwa na wanayamapori na kutuacha tukiwa hatuna chakula. Sasa hivi nalima ekari nne za alizeti napata magunia 25 mpaka 45 kama imezaa vizuri," alisema.

Ofisa Kilimo wa Kata hiyo, Neema Stamagunda, akielezea matokeo ya kilimo hicho, alisema kilimo cha alizeti kimebadili maisha ya kiuchumi kwa wananchi wake kwa kuongeza mapato,ajira, usalama wa chakula, ushirikiano na teknolojia na kuhifadhi mazingira.

"Alizeti imeanza kutoa fursa ya ajira Mairowa. Kilimo cha alizeti kinaweza kuunda fursa za ajira kwa watu wengi katika jamii, kutoka kwa wakulima hadi wafanyabiashara na wasindikaji.

"Lakini pia, suala la usalama wa chakula, limekuwa likiongeza uzalishaji wa alizeti, jamii ya huku inapata mafuta ya kula ya ndani, hivyo kupunguza utegemezi wa bidhaa za kigeni na kuboresha usalama wa chakula," alisema.

# Watu wenye uhitaji wakumbukwa X-Mas

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

WANACHAMA wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Endiamtu, Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, wamepeleka faraja ya sikukuu ya Krismasi kwa watoto yatima na wenye uhitaji maalum wanaolelewa na Kituo cha Light In Africa kilichopo Mji Mdogo wa Mirerani.

Jumuiya hiyo imetoa zawadi, ikiwemo nguo na vyakula ili kuwafariji wahitaji hao kusherehekea sikukuu kwa kula na kunywa.

Akizungumza baada ya kukabidhi misaada hiyo, Mwenyekiti wa Wazazi wa CCM Kata ya Endiamtu, Ernest Lukumay, alisema lengo ni kuhakikisha watoto hao wanasherehekea sikukuu ya noeli kwa furaha.

"Hatufahamu mwisho wetu hivyo ni vyema kuwakumbuka wahitaji kwa kutoa msaada pale tunapoweza ili kuwapa furaha watoto hawa," alisema Lukumay

Alisema jumuiya ya wazazi kata itakuwa inashiriki kwenye matukio mengi ya kijamii ili kuhakikisha wanatimiza vyema majukumu yao.


Katibu wa Wazazi wa Kata hiyo, Agrippina Paulo, alisema wametoa msaada kwa watoto hao ikiwemo nguo, mafuta ya kujipaka, mafuta ya kupikia, mchele na unga.

"Tumejitoa viongozi na wana jumuiya ya wazazi kupitia matawi na kata na wadau wengine tumeona tutoe msaada huu kwa watoto wa kituo hiki cha Light In Africa," alisema Agrippina

Awali, Mwenyekiti wa CCM, Tawi la Zaire, Jema Lilama, alisema wanawake wanaowasaidia watoto hao wanapaswa kupongezwa na kuombewa kwa Mungu.

"Hata huyu mama Mkurugenzi wa Light In Africa, ni mtu mwema mwenye kuwajali watoto kwani amejitoa mno katika kuwasaidia yatima na wenye uhitaji," alisema Lilama

Mmoja kati ya wasaidizi wa kituo hicho, Mariam Mbwambo akizungumza wakati wa makabidhiano hayo aliwashukuru waliotoa msaada huo kwa watoto hao.



# Watoto 32 wazaliwa mkesha wa Krismasi

**Na Timothy Itembe,** TARIME

WATOTO wapatao 32 wamezaliwa katika Vituo vya Afya 24 na Hospitali moja kwa njia ya kawaida katika mkesha wa Sikukuu ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo (Krismasi) wilayani hapa.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Dk. Amin Vasomana, alisema jana kuwa watoto 20 kati yao 11 wa kike na tisa wa kiume walizaliwa katika vituo vya afya 24 kwa njia ya kawaida.

Aidha, alisema wengine walizaliwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya hiyo ya Bomani kati yao, wa kike wakiwa sita na wa kiume watano.

Mganga mkuu huyo aliwataka wajawazito kuacha tabia ya kwenda kujifungulia kwa Wakunga wa kienyeji kwa sababu hao wanasababisha mfuko wa uzazi kupasuka badala yake wafike bila kuchelewa vituo vya afya vinavyotambulika.

**Mmoja wa kinamama waliojifungua usiku huo, Vicky Sebastian, mkazi wa Kijiji cha Mogabili, alisema alifika hospitalini hapo majira ya saa 4:00 asubuhi Desemba 23, 2024 na kupewa kitanda ilipotimu ...**

Mmoja wa kinamama waliojifungua usiku huo, Vicky Sebastian, mkazi wa Kijiji cha Mogabili, alisema alifika hospitalini hapo majira ya saa 4:00 asubuhi Desemba 23, 2024 na kupewa kitanda ilipotimu saa 8:00 usiku wa Desemba 25, 2024 alibahatika kujifungua mtoto wa kiume.

Mwanamama huyo alimpongeza muuguzi wa hospitali ya Bomani na kuwataka kuwa na kauli mzuri kwa wateja pindi wanapofika kupata huduma ya kujifungua.

Ofisa Muuguzi Msaidizi wa Hospitali ya Bomani, Esther Turuka, aliwataka wajawazito kuondokana na imani potofu ya kutumia dawa za kienyeji wakati wa ujauzito na kujifungua badala yake waende hospitalini mahala salama ili kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Ofisa huyo alitumia fursa hiyo kubainisha kuwa ndani ya hospitali yake wamezaliwa watoto 11 na kuomba serikali kuitazama hospitali hiyo hususani wodi ya wazazi na kuwaongezea vifaa vya huduma ya kujifungulia.



Baadhi ya akinamama waliojifungua usiku wa mkesha wa Krismasi wakiendelea kupatiwa huduma katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Bomani. **PICHA: TIMOTHY ITEMBE**

# AMCOS yatoa motisha ya pikipiki, wazalishaji wakubwa wa Tumbaku

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

VYAMA vya Msingi(AMCOS) vinavyolima Tumbaku katika Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, vimebuni mbinu mpya ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo kwa kutoa motisha ya pikipiki na baiskeli kwa wakulima wake wanaozalisha zaidi ili kuhakikisha wanafikia lengo la makisio wanayojiwekea kila msimu.

Mwenyeki wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Emmanuel Nyambi, aliyabainisha hayo juzi wakati akizungumza na vyombo vya habari namna walivyojipanga na kuhakikisha wanafikia lengo la kuzalisha kilo milioni 17 za tumbaku wakizingatia mkataba na makampuni yanayonunua zao hilo.

Alisema mbinu hiyo imebuniwa na Chama cha Msingi Ngokolo kutokana na uwepo wa mvua za wastani ili kuhakikisha wanafikia lengo la uzalishaji kulinganisha na msimu uliopita.

Nyambi alisema fedha zinazotumika zinatokana na ushuru wanaowatoza wakulima wake hivyo ni sehemu ya kurejesha kwao na kuvitaka vyama vingine kuiga mbinu hiyo ili kuongeza uzalishaji katika zao la pamba na tumbaku ambayo ndio chanzo kikuu cha mapato ya Ushetu.

Alisema msimu wa kilimo 2024/25 walifanya vyema katika uzalishaji wakichangia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Ushetu zaidi ya Sh.bilioni 65.98 na msimu ujao wanatarajia kuchangia zaidi kutokana na motisha iliyoibuliwa na vyama vya msingi na kuwasihi kuendelea kuzingatia maelekezo wanayopewa na maofisa kilimo.

Aidha, aliwataka viongozi wa vyama hivyo kubuni miradi ya kimaendeleo katika vyama vyao ili kuondokana na kutegemea ushuru pekee wa tumbaku na pamba hatua itakayowasaidia kujiendesha katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kuwa hayo ni maagizo kutoka wizara ya kilimo.

Mmoja wa wakulima wa tumbaku, Kulwa Shoto, alisema sababu nyingine inayowafanya wazalishe zaidi ni kutokana na bei kupanda kila mwaka kutoka dola 1.55 mwaka 2020 hadi kufikia wastani wa dola 2.38 mwaka 2024.

Aidha aliiomba serikali kuwapatia pembejeo na mbolea na kuhakikisha zinaendelea kuwafikia kwa wakati ili kufikia lengo la kilo wanazoingia mikataba na wanunuzi wao.

## Polisi yadaka 390 tuhuma mbalimbali

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mara linawashikilia watuhumiwa 395 wanaokabiliwa na tuhuma mbalimbali ikiwemo mauaji, wizi wa mifugo, uuzaji pamoja na usafirishaji wa dawa za kulevya katika msako uliofanyika mwezi Desemba, 2024.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Pius Lutumo, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema watu hao walinaswa katika operesheni maalumu kubaini na kudhibiti uhalifu wakati wa msimu wa sikukuu za mwisho na mwanzo wa mwaka.

"Operesheni hii imehusisha wilaya za Musoma, Butiama, Bunda, na Serengeti ambapo lita 2877 za pombe haramu ya Moshi (gongo) ilikamatwa sawa na wastani wa zaidi ya mapipa 10 ya lita 200 pamoja na mitambo 14 ya kutengeneza pombe hiyo," alisema SACP Lutumo.

Pia alisema walikamata kete 14,000 za bangi, mabunda 30 ya mirungi huku wakikamata makosa ya usalama barabarani 3,341 na baadhi ya kesi zilifikishwa mahakamani na wengine kulipa faini papo kwa papo.

Alisema jeshi hilo pia limekamata na kuokoa mali mbalimbali zilizokuwa zimeibwa ambazo ni pamoja na redio, televisheni, simu, kompyuta, mitungi ya gesi, pikipiki na injini ya boti.

SACP Lutumo alisema pia wanawashikilia na kuwahoji watuhumiwa wanane kwa tuhuma za kuvunja duka na kuiba usiku wa kuamkia Desemba 22, mwaka huu eneo la mtaa wa Kariakoo kata ya Bweri.

Kamanda Lutumi alitoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikina nao kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu hasa katika kipindi cha sikukuu ili zisherehekewe kwa amani na utulivu.



Ukurasa 13


Ukurasa 12

**MZEE BABA BALA**

## Fundi saa aliyetikisa jiji akihudumia vigogo, mageuzi teknolojia yamgeuza 'choka mbaya'

BUFE
IJUMAA DESEMBA 27, 2024
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Nipashe

# Pwani wamaliza mnada korosho wakiachiwa mabilioni mkononi

**Na Yasmine Protace, aliyekuwa Kibiti**


Shehena ya korosho, ikishushwa kwenye ghala mkoani Pwani.**PICHA:YASMINE PROTACE**

NI mnada wa nane na wa mwisho wa korosho uliofanyika Kibiti mkoani Pwani, tani 20,150 zimeuzwa kwa kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 60.

Akifunga mnada huo, Meneja wa Chama Cha Ushirika Mkoani Pwani (CORECU), Hamis Mantawela, anasema kuwa ni mnada wa mwisho wa korosho mkoani Pwani.

"Tumefanya minada nane ya korosho katika mkoa wa Pwani, ambapo mpaka sasa tumefanikiwa kuuza tani 20,150 kwa jumla ya Sh. bilioni 65," anasema.

Anaongeza kuna wakulima wa zao hilo hawajalipwa pesa zao na kwamba, kama ilivyo minada ya nyuma, kuna wakulima hajalipwa malipo yao, akiitaja kuwa changamoto kwa baadhi yao, huku kukitajwa taarifa zao za kibenki hazikuwa nzuri.

Mantawela anasema kwamba, pamoja na changamoto hiyo,wamewaelewesha wakulima utaratibu wa kufanya, ili walipwe haki zao.

Pia, anataja minada yote imeenda vizuri na wakulima walipata pesa zao kwa wakati, huku bei ya korosho katika minada ya kwanza; mazao ya daraja la kwanza iliuzwa kwa kilo zaidi ya shilingi 3,000, huku daraja la pili iliuzwa kilo moja kwa bei, zaidi ya shilingi 2000 .

"Kadiri minada inapozidi kufanyika, korosho ziliuzwa kwa kilo zaidi ya shilingi 2000," anafafanua Mantawela, akiongeza kuwa bei hizo bado ni bei nzuri, tofauti na bei za miaka ya nyuma.

Katika hilo, anaipongeza serikali kwa kuandaa mfumo wa uuzaji korosho kwa njia ya mtandao, ambao umeenda vizuri, ikiwamo kufanikisha wanunuzi kujitokeza kwa wingi.

Pia, anaongeza kuwa maelekezo ya serikali yalitaka wakulima walipwe pesa zao moja kwa moja bila ya kupelekwa katika vyama vya ushirika.

Anasema, pia kuna kasoro katika malipo ya kibenki, akitaka wakulima walioingiziwa pesa kimakosa kwa mfumo huo warudishe.

"Kuna changamoto imejitokeza ambayo baadhi ya wakulima waliingiziwa pesa mara mbili kimakosa, inatakiwa wazirudishe," anasema.

Anaongeza kuwa, wamepigiwa simu ili warudishe na wapo waliorudisha, baadhi wakibainika kuwa na elimu duni ya taratibu za kibenki.

Mwenyekiti wa CORRECU mkoani Pwani Mussa Mng'eresa, anasema huo ni mnada wa mwisho wa korosho katika mkoa huo.

Anaahidi kwamba, elimu itaendelea kutolewa, ili kuendeleza wakulima wazalishe korosho kwa kiwango, daraja la kwanza.

Anashauri kama kuna wakulima ambao hawajalipwa, wafuatilie ili walipwe haki zao. Pia, anataja kuwa mbegu za zao la ufuta na mbaazi zitatolewa, kwa wakulima ili waanze kulima mazao hayo

**MZIZI WA KINACHOVUNWA** Ilikuwa mwaka 2018, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa Pwani Evarist Ndikilo, wakati wa uzinduzi wa upandaji wa mikorosho mipya uliofanyika katika shamba la Ruvu JKT mwanzoni, akatamka:

"Napenda kutoa rai kwa wakulima wote wa korosho mkoa wa Pwani, kuwa waende katika shamba darasa la Ruvu JKT, kwa ajili ya kujifunza namna ya upandaji wa miche ya korosho ya kisasa.

Akaitaja ni mojawapo ya mazao ya biashara ya kimkakati nchini, ikiwa katika kiwango cha juu kuliingizia taifa fedha nyingi za kigeni.

Pia akasema kuwa, serikali kupitia bodi ya korosho Tanzania, wakati huo ikatoa kilo 7,182 za mbegu bora za korosho kwa mkoa wa Pwani na kuzisambaza katika halmashauri zake zote.

Mbegu hizo zilikadiriwa kuzalisha miche bora 1,039,687 ya korosho, ambayo ikatolewa bure kwa wakulima.

Leo hii, imepita miaka sita, ikiwa katika matarajio ya kuing'arisha Pwani na korosho bora zinazofika sokoni kila msimu, iking'ara kwa daraja la kwanza pale inapotunzwa vizuri.

Ndikilo akawataka viongozi wa wilaya na halmashauri wakati huo, wasimamie vizuri mchakato wa ugawaji wa miche hiyo, na taarifa za wakulima waliokabidhiwa miche hiyo ya korosho zihifadhiwe vizuri kwa ajili ya ufuatiliaji.

Aidha akawataka maofisa ugani wa halmashauri za mkoa huo wa Pwani, watoke maofisini, kwenda kwa wakulima kwa ajili ya kutoa elimu na kanuni za kilimo bora cha korosho.

Wito wake alioutoa wakati huo, bado unabaki kuwa msingi na falsafa katika uzalishaji korosho hadi sasa na aliutamka kuwa:

"Ningependa kutumia fursa hii kuwakumbusha na kuwatahadharisha viongozi wa (AMCOS) kubadilika na kama hawatakuwa tayari kubadilika na kusimamia mfumo uliowekwa kulingana na sheria ni afadhali wajivue wenyewe uongozi na tutawachukulia hatua kali za kisheria."

Aidha, Ndikilo akawataka wawekezaji wa viwanda kuvijenga vya kubangua korosho na vinavyotengeneza magunia ya kuhifadhi korosho nchini, kuepuka adha ya kuagiza magunia kutoka nje ya nchi.

IJUMAA DESEMBA 27, 2024 BUFE 13

BIASHARA

MZEE BABA BALA

# Fundi saa aliyetikisa jiji akihudumia vigogo, mageuzi teknolojia yamgeuza ‘choka mbaya’

- Wateja wake wafanyabishara, wazito wenye simu za Mil. 24/-
- Karithi stadi za baba, aliyevuka mipaka kutumikia ujuzi huo

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA jiji la Abuja, nchini Nigeria, kuna duka la kutengeneza saa la Bala Muhammad. Hapo kuna fundi saa maarufu anayejulikana kwa jina, Baba Bala.

Katika zama hizo teknolojia haijakua, alikuwa maarufu maradufu, huku mwenyewe ‘akikusanya’ pesa ndani na nje ya mipaka kwa ufundi wake huo.

Duka hilo liko katikati ya barabara kuu ya Kaduna, jijini Abuja, mtaa maarufu uliojaa maduka ya vifaa vya ujenzi na ndani yake kulikuwa na saa nyingi zilizozunguka kila kona, kila moja ikionesha muda wake.

Hapo fundi huyo, ambaye sasa ana umri miaka 68, ametulia kwenye kiti kidogo kilichozungushwa na meza yake ya kazi.

Baba Bala, alikumbuka enzi zilizopita alipokuwa akitengeneza saa kwa haraka, wakati aliokubaliana na wateja wengi waliokuwa wanamletea saa zao kurekebishwa.

“Kuna wakati nilikuwa napokea zaidi ya saa 100 kwa siku moja,” anaelezea, akionesha jinsi biashara yake ilivyokuwa na umaarufu mkubwa.

Anasema, leo, anakumbwa na wasiwasi mkubwa akitamka kwa kulalamika: “Teknolojia mpya, hasa simu za mkononi, zinauwa biashara yangu.”

Mzee huyo anakiri kazi aliyojivunia kwa miaka mingi ilikuwa ikielekea ukingoni na kwamba maarifa aliyopata kutoka kwa baba yake na nduguye mdogo, yanaanza kupotea umuhimu wake.

Baba Bala anaeleza jinsi alivyofikia hatua hiyo, baada ya kufundishwa na baba yake, Abdullahi Bala Isa, aliyejulikana fundi wa saa maarufu katika miji mingi ya nchi za Afrika Magharibi.

Baba yake Bala, ana historia ya kusafiri maeneo kadhaa Magharibi mwa Afrika kwa zaidi ya miezi sita kuanzia, Senegal hadi Sierra Leone, kwenda kufanya kazi moja; kutengeneza saa za watu zilizoharibika.

Kuna wakati Baba Bala alikuwa akiishi jiji kuu la Nigeria, wazito na wanasiasa wa mahali alikoishi, alikuwa fundi wao akiwatengenezea saa zao na daima ‘hakulala’ akitajwa kuwa na kipato kinachojitosheleza.



Fundi Baba Bala, akiwa kazini.

Ana simulizi ya kukumbuka maofisa wakuu wa serikali, walikuwa wakimletea saa zao za mikononi aina ya Rolex zenye thamani ya Dola za Marekani 10,000 (sawa na Sh. milioni 24).

Anasema, saa aina hizo huwa zinapendeza na ndio maana anavutiwa zikiitwa ‘saa kutoka Uswisi’, yeye naye ‘hajambo’ mkononi akiwa na saa nyingine kutoka Uswisi aina ya Longines, akihusudu hata analala nayo.

“Nikitoka nyumbani kwangu nikumbuke sijavaa saa yangu, hunibidi nirejee nyumbani. Hakika siwezi kukaa bila saa yangu - ina umuhimu kwangu,” anaeleza fundi Bala

**BABA KAMA MWANA**

Katika duka lake amening’inizia picha kubwa ya baba yake,Abdullahi Bala Isa, aliyopigwa akiwa ofisini mwake kabla ya kifo chake mwaka 1988.

Marehemu Mzee Isa, anajulikana sana kwa umahiri wa kurekebisha saa zilizoharibika katika maeneo mengi kama vile Freetown, Sierra Leone na Dakar, Senegal, hakushindwa hata vile vilivyoshindikana,akitatua na kuna wakati alikuta mrundikano wa saa.



Bidhaa saa zikiwa dukani kwa Baba Bala.

Baba Bala, anasema wote hawajui baba yao alikotoa ujuzi wa kutibu saa mbovu, kukiwa na tetesi aliunasa enzi za ukoloni wa Muingereza, nchini mwao.

Fundi Bala akiwa mzaliwa wa miaka minne kabla ya Nigeria kupata uhuru mwaka 1960, ana nyongeza baba yake katika simulizi:

“Babangu alikuwa mtaalam wa kutengeneza saa na alikuwa akisafiri maeneo mengi kuunda saa. Alijifunza nikiwa mdogo na nikaamua kufuata nyayo zake nilipoinukia ukubwani.”

“Mimi nilianza kuwa fundi wa saa nilipokuwa na umri wa miaka kumi,” anakumbuka Baba Bala, akieleza jinsi alivyovutiwa na taaluma ya saa tangu utotoni.

**KUTOKA SHULE**

Anajigamba: “Wakati wenzangu walikuwa wanalia kwa kutokuwa na pesa, mimi nilikuwa na pesa kwa sababu nilikuwa nikifanya kazi.”

Anasema ni umahiri uliomvutia hata mwalimu wake akiwa shuleni, akiwa na simulizi: ‘Mwalimu alikuwa na saa ambazo zimeharibika.

“Alikuwa amejaribu kuzipeleka kwa fundi zitengenezwe. Lakini haikuwezekana, aliponijulisha hayo, alinipatia saa zake na nikamtengenezea siku hiyo hiyo.’’

Fundi huyo anaeleza, saa zilikuwa zikitambulika kama mavazi ya kila siku - ilikuwa ni vigumu kuona mwanaume ambaye hajavaa saa ya mkononi.

Watu wengi walikuwa wakileta saa zao zitengenezwe na baadhi yao hawarudi kuzichukua. Maisha ya Baba Bala yalianza kubadilika, kama ilivyokuwa kwa wateja wengi wa zamani.

“Leo, vijana wanatumia simu kutafuta majibu badala ya saa,” anaeleza wakati ambao biashara yake ilijulikana na kwa matajiri na viongozi wa kiserikali.

Analalamika sasa ni vigumu kupata wateja wapya, akitamka kwamba “saa za kisasa zinageuza kila kitu.”

Mtaani hapo anakopatikana anasema, maduka ya saa eneo la Kaduna, maduka mengi yamefungwa na baadhi ya marafiki zake wameshajiuzulu au wamefariki.

Lakini Fundi Isa Sani (65), mfanyabiashra mwezake naye bado anaendelea na biashara ya kutengeneza saa zilizoharibika .

‘Nikienda dukani kwangu kila siku, hukaa bila kupata mteja yoyote siku nzima, lakini bado sijakata tamaa tangu mwaka 2019,’’ anasema.

‘’Nina shamba ambalo watoto wangu hunisaidia kulima na tunajikimu kimaisha kupitia mavuno ya shambani,’’ anasema.

Kwa unyonge, anasema: ‘’sifikirii kuwa kurekebisha saa zilizoharibika itakuwa biashara ya kunoga kama awali.’’

**WADAU MTAANI**

Vijana wa eneo hilo, kama Faisal Abdulkarim na Yusuf Yusha’u walio na umri wa miaka 18, wanakubali kwamba siku hizi, simu za mkononi zimechukua nafasi ya saa.

“Nikiangalia simu yangu, naweza kujua muda kwa urahisi,”anasema mmoja wao.

Dk. Umar Abdulmajid, Mhadhiri wa Chuo cha Mawasiliano cha Yusuf Maitama anaamini mambo yatabadilika, akiwa na kauli:

‘’Saa za zamani hazipo tena kwa hivyo, hakuna shughuli ya kuzirekebisha, lakini kuna saa zinazotumia intaneti zimeanza kuingia kwahivyo zitahitaji fundi wa kuzitengeza zikiharibika.’’

Baba Bala anakubali mabadiliko hayo, lakini akijua anapitia changamoto kubwa.

“Simu na teknolojia ya kisasa vinafifisha biashara yangu, lakini mimi bado nipo hapa na nitaendelea kutoa huduma,” anasema, akieleza kuwa biashara yake inahitaji kubadilika ili kuendana na wakati.

Baba Bala hutumia muda mwingi katika duka lake akisikiliza habari kwa njia ya redio

“Watu wengi wamekuwa wakileta saa zao zitengenezwe na baadhi yao hawarudi kuzichukua zimejaa hapa,’’ anasema Baba Bala.

Lakini Baba Bala amekataa kufunga duka lake,- mtoto wake wa kike ambaye huuza nguo na humnunulia kadi za simu, angalau auze apate kipato cha siku.

Hata hivyo, anajivunia kuona mtoto wake wa kiume mwenye umri wa miaka 12 akitaka kuwa rubani, na alifurahi kuona familia yake inavyoendelea kuona dunia kwa mtazamo tofauti.

**Kwa mujibu wa BBC**



Fundi Baba Bala, akiwa na picha ya marehemu baba yake, fundi saa wa kimataifa, aliyemrithisha ujuzi huo.
**PICHA ZOTE: MTANDAO.**

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Karibu 2025, ila wafanyabiashara msipandishe bei bidhaa, tunaumia!






NA SABATO KASIKA

SIKUKUU ya Krismasi imemalizika sasa inafuata Mwaka Mpya wa 2025, ambayo kama Mwenyezi Mungu atatujalia kuwa hai, tutaisherehekea Jumatano ijayo. Ni kama siku tano zijazo.

Kwa wale ambao tumebahatika kuifikia Krismasi, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ulinzi wake kwetu kila uchao, kwani wapo baadhi yetu ambao walitangulia mbele ya haki siku chache kabla ya sikukuu hiyo.

Tunapokaribia kufikia mwaka mpya, ninaomba nitumie nafasi hii kuwatakia sikukuu njema yenye baraka tele na amani, mle mnywe lakini kwa kiasi.

Lakini pamoja na hayo, ninapenda kuwakumbusha wenzetu wafanyabiashara, kuepuka kupandisha bei vitu na kusababisha watu kushindwa kumudu bei.

Mtindo huo ambao umekuwa ukijirudia kila wakati wa sikukuu, ni mwiba kwa watu wa kipato kidogo ambao hudunduliza pesa, ili angalau wakati wa sikukuu wale vizuri na wawe sehemu ya kicheko hicho .

Ingependeza kama wakati wa sikukuu, tukaona bidhaa nyingi katika maduka ingekuwa zinapunguzwa, ili kuwawezesha watu wote kumudu kununua mahitaji na kufurahia sikukuu hiyo.

Wakati wa Sikukuu ya Krismasi, tumeshuhudia wafanyabiashara wa nyama wakipandisha bei kutoka shilingi 10,000 kwa kilo hadi kufikia shilingi 12,000. Hiyo ni bei ya Dar es Salaam, lakini tumeambiwa katika vyombo vya habari nyendo ni hizo, kupanda bei kila kona, kulingana na wastani wake.

Hapo tuweke nukta kutafakari, jamani wa hali ya chini wataserebuka vipi?

Kwa mtindo huo ni kwamba wale ambao hula nyama mara moja kwa kulingana na kipato chao, hawawezi kumudu bei hiyo.

Ni vyema wakati kama huo, ndio ambao bei za bidhaa zingekuwa za kawaida kama njia mojawapo ya wafanyabiashara kuonesha kuwa wanawajali wateja wao wenye uwezo wa kipato na wa kawaida.

Ninadhani kipindi cha sikukuu kisingetumiwa na baadhi ya wafanyabiashara kujinufaisha zaidi, bali wawajali wateja wao bila kuangalia uwezo wa kipato au kujali maslahi makubwa tu.

Ikumbukwe kuwa msimu wa sikukuu ndio ambao kila mtu hujitutumua nyumbani kwake kinapikwa chakula kizuri, watoto wanatoka na nguo mpya, hivyo ingependeza kama hawataumizwa na bei ya bidhaa madukani.

Lakini mtindo wa kuvizia msimu wa sikukuu na kupandisha bei ya bidhaa, ni sawa na kukomoa watu sasa wafanyabiashara walione tatizo hilo na kulitafutia ufumbuzi haraka ili kuwapa unafuu wateja wao.

Inaumiza kuona, kitu ambacho ulinunua jana kwa shilingi 8,000, unakuta leo kinauzwa shilingi 10,000. Kwanini bei ipande ghafla kiasi hicho, kuna nini hapo katikati?

Ni kweli bidhaa itapanda na wateja watakuja tu, lakini kumbukeni kuna kundi lingine nyuma linakwama kupata mahitaji ya sikukuu kutokana na bei ya bidhaa kuwa juu.

Jambo la kuzingatia ni kwamba wale wote wanaofanya biashara iwe kubwa au ndogo, wasitumie mwanya huo kujinufaisha au kuufanya msimu wa sikukuu kama kipindi cha mavuno kwao.

Ninaamini kila mmoja awe na uwezo mkubwa au mdogo kifedha, anatamani angalau siku ya sikukuu ajitutumue anunue chochote atumie na familia yake.

Vilevile, huyo anayejitutumua na mwanzo wa mwaka, ndiye mhanga wa janga la gharama za lazima, ikianzia na kinara wao ada na gharama za shule kwa wanafunzi.

Hivyo, enyi wafanyabiashara na mamlaka zinazohusika pale inapobidi, tumieni uungwana kuhakikisha mnachangia kuzuia mfumuko wa bei wa ghafla ambao husababisha maumivu kwa baadhi ya watu hasa wa kipato cha chini.

Wafanyabiashara wakubwa, wadogo na wachuuzi wote tunaelekea katika sikukuu ya mwaka mpya, muangalie uwezekano wa kuhakikisha kila mteja anapata anachokitaka kulingana na uwezo wake kiuchumi.

Niwatakie maandalizi mema ya sikukuu ya Mwaka Mpya, uwe wa heri na fanaka, atakayejaliwa kufikia, atimize yote mema aliyokusudia kuyafanya kwa mwaka 2025.

o

UCHUMI

WALIOPATA MIMBA KURUDI SHULE...

# Chimbuko la hatua kimataifa hadi nchini, ubunifu wake Samia, safari ya utekelezaji

**Na Christina Haule, MOROGORO**



Mhitimu wa Diploma ya Unesi na Ukunga, akiwa kati ya wanafunzi waliosomeshwa na mradi wa kurejeshea ndoto mabinti. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE •**

MNAMO Mei mwaka huu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiwa bungeni jijini Dodoma, akasema serikali inatunga sheria na kanuni kurejea shule wanafunzi waliopata ujauzito, isiwe hiyari ya mtu.

Ni taarifa iliyopokewa kwa furaha na asasi za kimataifa, ikiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) tawi la Tanzania, lililoenda mbali kuipongeza serikali nchini

Hicho kilichonenwa na Mtendaji Mkuu wa Serikali, Waziri Mkuu, kikafafanuliwa tena na mkuu wake aliyemwelekeza, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa ziarani mkoani Geita mwaka huu.

Kauli yake ilikuwa: "Tumeamua, watoto wote ambao wameacha shule kwa sababu mbalimbali utoro, sababu za kisheria kwamba, ukipata mimba huwezi kuruhusiwa kuendelea na masomo.

"Wale waliodondoka darasa la saba, tunajua kuna wanafunzi wetu wazuri sana, kwa bahati mbayá wakati wa mtihani

"Mtihani ni mtihani, hawakufanya vizuri, lakini baada ya kukaa nje wamejutia tunawapa nafasi nyingine kurudi na na kufanya mtihani. Lengo la uamuzi huu ni kutoa fursa pana," akatamka Dk. Samia.

Wakati hilo linafanyika nchini, lina mizizi mrefu kimataifa, ukiwa na miaka 33 barani Afrika, ikianzia nchini Zimbabwe wakati huo 1991, taifa hilo lina miaka 10 ya uhuru.

Ni hatua ambayo ina unasaba na nchini, kwani uhuru na nyendo za maendeleo ya Zimbabwe, mzizi wake uko Tanzania.

Katika historia hiyo, taasisi isiyo ya kiserikali iitwayo Camfed, ilianzishwa kwa lengo la kumkomboa mtoto wa kike, kuondokana na shughuli za shambani na jikoni nchini humo.

Hata kutimu umri miaka 14 mnamo 2005, Mkurugenzi wa asasi Camfed tawi la Tanzania, Nasikiwa Duke, anasimulia ukaanzishwa ubunifu huo wa Zimbabwe, baadaye ukaendelezwa katika nchi za, Malawi, Ghana na nchini Tanzania ilikoanza na kikundi cha wasichana 28.

Hapo kunaelezwa, baadaye wakaungana kuanzisha kikundi kinaitwa Mfumo wa Malezi kwa Kuwapokea Wenzao na Kuwalea (CAMA) wakitokea mikoa ya Iringa, Morogoro, pia wilaya za Rufiji na Kibaha, mkoani Pwani.

Nyenzo hiyo ambayo Rais Dk. Samia sasa anaiweka kisheria, Duke anasema mwaka 2006 wakaanzisha Camfed-Tanzania iliyoanza na shule za msingi kutoka wilaya nne za maeneo hayo yalikoasisiwa hali mbaya.

Anataja jumla yao wakiwapo wasichana 28,000, lakini kufika mwaka huu unaofikia ukomo, kuna wasichana 57,000.

Duke anasema kwa sasa wamefikia shule 365 za serikali ndani ya halmashauri 35 kitaifa, akisema kinachofanyika wanaendeleza kile anachohimza Rais Dk. Samia na mtendaji wake mkuu kiserikali, Majaliwa.

Anarejea sehemu ya takwimu zao, kati ya mwaka 2006 na 2010, walihudumia wanafunzi 1000, kwa gharama ya shilingi 350,000 kila.

### MABINTI WAWEZESHWA

Duke anasema mwaka 2013, wakaanzisha utaratibu wa kuwajengea uwezo kimaisha wasichana kutoka shule 360; ila kwa sasa wana shule 400 katika shule za wilaya zaidi ya 35 walizokuwa nazo baada ya Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa - TAMISEMI) kuwapatia fedha, hata wakafikia wilaya 41.

Anautaja mpango huo unawasaidia wanafunzi wa kike, lengo ni kufikia mabinti 60,000 wa sekondari za serikali, kuhakikisha wanawasimamia na kumaliza shule, hata binti kufikia elimu ya juu.

Anasema kutokana na umuhimu wa elimu kwa mabinti wameamua kuwasomesha kuanzia kidato cha kwanza hadi chuo kikuu, tayari wamewezesha mabinti 5,218 kusoma vyuo vikuu na kwa mwaka huu 2024 wanafunzi 604 wapo vyuoni wanasoma.

Binti Asha Mang'ombe (23), anatamka kufanikiwa kupata elimu ngazi ya Diploma ya Unesi na Ukunga, akiwa sehemu ya mabinti wanufaika 57,000, katika kazi hiyo.

Mang'ombe anasema, mwaka 2015 alianza kuhudumiwa na Camfed kuanzia kidato cha kwanza, baada ya wazazi wake kukosa uwezo wa kumsomesha kutokana na ugumu wa maisha.

Mang'ombe anasema, baada ya kuhitimu diploma yake Agosti mwakia huu, anasubiri kupata leseni ya fani yake.

### KAULI ZA KISERIKALI

Mkurugenzi Udhibiti Ubora wa Shule, kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Ephraim Simbeye, anaipongeza Camfed kutambua nafasi ya mtoto wa kike kufikia elimu inayokusudiwa, wakiwashika mkono kuhakikisha wanafikia ndoto zao.

Anasema, Wizara ya Elimu imejikita katika utekelezaji wa sera na mtaala ulioboreshwa wa mwaka 2014 toleo la 2023, wakitoa usimamizi na utekelezaji mtaala huo na elimu ya amali kwa wanafunzi hasa, sekondari.

Simbeye anasema, sera na mtaala huo ukitekelezeka vyema, wanafunzi watafika nao mbali, hata kuinua elimu kitaifa.

Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Watu Wazima na Elimu Maalum, Ernest Hinju, anasema suala la kusimamia watoto wa kike kwenye elimu, lilianza mapema Rais Dk. Samia alipoelekeza kuwarudisha shuleni wasichana waliopata mimba, kupitia elimu mbadala.

Anataja jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita katika kumkomboa mtoto wa kike, zimeeendelea kuzaa matunda na kuna jumla ya wanafunzi 1692 kati ya 28,971 wa shule za sekondari nchini, waliopata ujauzito na kusitishwa masomo mwaka 2017 hadi 2021/2022, wamerudi na kuendelea na elimu ya sekondari.

### CHANGAMOTO ZILIVYO

Mkurugenzi Duke anataja changamoto zao zimo ajira wameweza kuajiri asilimia 43 ya wafanyakazi hao ndani ya CAMFED na kusaidia gurudumu la maendeleo ya miradi kwa Camfed na kuwasaidia wasichana kwa manufaa yao binafsi.

Anasema kati ya mabinti 57,000 waliosomeshwa na Camfed, asilimia 37 wana nafasi za uongozi kwenye maeneo yao walikotoka, wakiwamo maofisa watendaji wa kata na vijiji, madiwani na wenyeviti wa vijiji.


Aidha anasema wameanza kuwasaidia wahitimu wa kidato cha nne na waliopo vyuoni, wakiwapa miradi ya ujasiriamali kuanza na mitaji ya shilingi 200,000 kwa kila mmoja.

Duke anasema, kupitia mafunzo ya biashara, mitaji na mikopo wametengeneza ajira 2,307 za kudumu na za muda mfupi, sambamba na kuanzisha biashara 15,475 mbalimbali, ikiwamo maduka.

Jitihada za serikali ya Awamu ya Sita katika kumkomboa mtoto wa kike, zimeeendelea kuzaa matunda na kwamba wanafunzi 1692 kati ya 28,971 wa shule za sekondari nchini waliopata ujauzito na kusitishwa masomo mwaka 2017 hadi 2021/2022, wamerudi na kuendelea na elimu ya shule ya sekondari.

Tamko hilo la kiserikali kuhusu kurejeshwa tika mfumo rasmi wa shule watoto wa kike waliopata ujauzito wakiwa shuleni, lilipokewa na umma kwa shauku nchini, ikitumika ndani yake kuzingatia haki nne za mtoto; kuishi, kuendelezwa, kulindwa na kushirikishwa.

Uamuzi huo uko katika Waraka i wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia nchini, uliotangazwa Novemba mwaka 2021, wakati Rais Dk. Samia ana wastani wa zaidi ya nusu mwaka katika nafasi hiyo.



Mdau wa harakaki kurejeshea ndoto mabinti waliopata ujauzito masomoni, Nasikiwa Duke.





# Adaiwa kutoa huduma tiba bila vyeti

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

MAISHA ya wakazi wa kitongoji cha Kashamawele kata ya Kitaraka, Halmashauri ya Itigi, wilayani Manyoni mkoani Singida, ziko katika hatari baada ya mtu mmoja kutumia nyumba yake kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wakiwamo wajawazito huku akiwa hana taaluma ya udaktari.

Mtu huyo aliyefahamika kwa jina moja la Charles ambaye alikimbia baada ya kuwaona maofisa wa serikali, alibainika kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa kwa kutumia dawa hata ambazo zimeisha muda wake.

Daktari huyo feki alibainika baada Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Itigi, Dk. Emmanuel Mallange, kufanya ziara ya kushtukiza katika kitongoji hicho akiwa na maofisa wengine wa serikali.

Dk. Mallange akizungumza na wananchi wa kitongoji hicho, alisema daktari huyo feki amekuwa akitoa huduma nyumbani kwake zikiwamo za kulaza wagonjwa hali ambayo ni hatari kwa kuwa hana taaluma ya udaktari.

"Wananchi acheni kwenda kupata huduma kwa Charles. Huyu si daktari mmejiaminisha naye na baadhi mnamtetea hapa tutakuwa tunaua wagonjwa. Kwanza anatumia dawa zingine ambazo zimeisha muda wake. Anahudumia hadi kinamama wajawazito, hii haikubaliki," alisema.

> **"Wananchi acheni kwenda kupata huduma kwa Charles. Huyu si daktari mmejiaminisha naye na baadhi mnamtetea hapa tutakuwa...**

Dk. Mallange alisema mtu huyo Julai, mwaka huu, Halmashauri ya Itigi ilifunga duka la dawa muhimu alilokuwa akilimiliki katika kitongoji cha Kashamawele ambalo lilikuwa likiendeshwa bila kusajiliwa,kufanya upasuaji wagonjwa na kuuza dawa ambazo muda wake wa matumizi umepita.

Alisema daktari huyo feki baada ya kufungiwa duka, aliamua kufungua hospitali kinyemela nyumbani kwake ambako anatoa huduma kwa wagonjwa.

Dk. Mallange alisema kama mtu huyo anapenda kutoa huduma za matibabu ajenge hospitali ambayo itakaguliwa na kuwaajiri watu waliosomea udaktari badala ya kutoa huduma kinyemela hali ambayo ni hatari kiafya kwa watu wanaopatiwa matibabu.

Julai, mwaka huu, duka la mtu huyo lilipokaguliwa lilikutwa na dawa ambazo hazitakiwi kuuzwa dukani ikiwa ni pamoja na dawa za usingizi sambamba na dawa zilizo pita muda wake wa matumizi.

Mmiliki wa duka hilo alikuwa akijitambulisha kwa wananchi kuwa yeye ni daktari na amekuwa akitoa huduma mbalimbali zikiwamo za upasuaji mdogo na kulaza wagonjwa.



Mkuu wa Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Moses Machali, (aliyevaa koti jeusi na shati jeupe) akiwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Said Kalima, wakifanya ukaguzi wa ujenzi wa shule ya sekondari ya Kidarafa inayojengwa kata ya Mwanga wilayani humo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wanawake wenye ulemavu wajengewa uwezo kushiriki uongozi, ujasiriamali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Foundation For Disabilities Hope (FDH) ya mkoani Dodoma, imeanza kuteleza mradi wa mwaka mmoja wa kuwajengea uwezo wanawake wenye ulemavu kushiriki masuala ya uongozi pamoja na ujasiriamali ili kuwainua kiuchumi.

Mradi huo wa mwaka mmoja unaolenga kuimarisha masuala ya usawa wa kijinsia utawafikia wanawake wenye ulemavu zaidi ya 300, katika kata mbalimbali za halmshauri ya wilaya ya Kondoa.

Mkurugenzi Mtendaji wa FDH, Michael Salali, akizungumza wakati wa utoaji wa mafunzo kwa walengwa wa mradi huo wilayani hapa alisema mradi huo wa mwaka mmoja umejikita kusaidia watu wenye ulemavu kukamata fursa za kiongozi pamoja na ujasiriamali.

Alisema, takwimu zinaonesha ushiriki wa watu wenye ulemavu kwenye masuala ya uchaguzi mbalimbali nchini bado ni hafifu hali ambayo inahitaji jitihada za pekee kuibadili.

"Hata katika uchaguzi uliopita wa Serikali za Mitaa hivi karibuni takwimu zinaonesha kuwa ushiriki wa watu wenye ulemavu ulikuwa mdogo lakini pia hata ushiriki wa wanawake ulikuwa hafifu sana, hivyo kuna haja kwa wadau pamoja na serikali kuweka jitihada kubadili hali hii.

"Tutakua hapa kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuwaelimisha na kuwajengea uwezo wanawake wenye ulemavu waweze kushiriki kikamilifu katika michakato mbalimbali ya kiuongozi niwashukuru sana Abilis Foundation kwa kufadhili mradi huu ili kuongeza elimu na uelewa kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu ili kuwa na jamii jumuishi," alisema

Pia alisema wanaishukuru serikali ya wilaya ya Kondoa kwa kuwapa ushirikiano ili kuwafikia na kuwajengea uwezo watu wenye ulemavu ili kila mtu mwenye ulemavu nchini asonge mbele.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Kondoa, Jafari Haji, alisema mradi huo umekuja wakati mwafaka kwani watu wenye ulemavu bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ushiriki wa masuala ya uongozi.

"Mafunzo ambayo yanayotolewa kupitia mradi huu yatasaidia watu wenye ulemavu kushiriki kwenye masuala mbalimbali yakiwemo ya kiungozi pamoja na ujasiriamali," alisema.

Salma Ramadhani, mkazi wa Kondoa, alishauri wazazi kuacha tabia ya kuficha watoto wenye ulemavu bali wawatoe ili wapate haki zao za msingi ikiwemo elimu.

# Mchungaji akemea uharibifu sikukuu mwisho wa mwaka

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATANZANIA wameombwa kudumisha amani na utulivu wakati wa kusherehekea sikukuu za mwisho wa mwaka kwa kujiepusha na vitendo viovu vikiwamo uharibifu wa miundombinu iliyoigharimu serikali fedha nyingi.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mchungaji Kiongozi, Joseph Masinga wa Kanisa la (PHAMT) Bethel Nzunguni, Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Mchungaji Masinga alisema Watanzania wanapaswa kujiepusha na vitendo viovu vinavyoweza kuondoa amani na upendo.

Alisema sikukuu isisherehekewe kwa vitendo ambavyo vinavyomchukiza Mungu kama unywaji wa pombe, uzinzi na ukatili dhidi ya watoto, wazee na wanawake.

"Ni vyema tunaposherehekea tumaanishe kwa kujiuliza tunafanya hivyo kwa maana gani na hili tutafanikiwa ikiwa tu tutasherehekea kwa amani,upendo na mshikamano wa pamoja," alisema

Pia aliiomba jamii katika sikukuu hizi kujumuika pamoja na watu wasiojiweza kwa kuwapatia misaada mbalimbali ili iweze kuwapunguzia ukali wa maisha.

"Dini nzuri ni ile ya kuwasaidia watu wenye mahitaji, hivyo niwaombe kwenye kusherehekea sikukuu hizi tuungane kwa pamoja kwa kushirikiana na wenzetu wenye uhitaji," alisema

Hata hivyo, aliwataka Watanzania mwaka 2025 ambao utakuwa wa uchaguzi, kumwomba Mungu, ili wapate viongozi watakaokuwa na mapenzi juu ya nchi yao.

Alisema kama ambavyo walikuwa wakiomba mwaka 2024 kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, hivyo hivyo wanapaswa kuongeza maombi ili kuwapata viongozi hao.



# DC aonya matumizi mabaya mikopo

**Na Elizabeth John,**
WANG'ING'OMBE

MKUU wa Wilaya ya Wang'ing'ombe, Zakaria Mwansasu, amevitaka vikundi vilivyonufaika na mikopo ya asilimia 10 wilayani hapa, kuzitumia vyema fedha hizo kwa malengo mahususi na si za kuongeza mume wala mke.

Mwansasu aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi 118 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyopata sifa ya kukopeshwa uliofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Wang'ing'ombe.

Mwansasu alisema kwa kuwa vikundi hivyo vimeomba mkopo kwa kuandika malengo mahususi basi zikafanye kazi iliyokusudiwa na si vinginevyo.

"Hizi fedha si za mboga, si fedha za kwenda kulipa ada ya mtoto, si fedha ya kwamba sasa nimeipata kutoka kwenye kikundi si ya kwenda kuongeza mke au mume. Si fedha ya kwamba nakwenda kununua nguo na si fedha ya kwenda kuichezea," alisema.

Mwanasasu alisema huo ni mkopo ambao hauna riba, hivyo aliwataka kuhakikisha watakapozipokea wazipeleke kwenye mahitaji ambayo yamekusudiwa ili kurejeshwa kwa wakati.

"Na kikundi kikishindwa hili niliseme wazi kikishindwa kurejesha zipo sheria ambazo zimetungwa kwa ajili ya kukiwajibisha hicho kikundi," alisema Mwansasu.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) Afya, Festo Dugange, ambaye pia ni Mbunge wa Wang'ing'ombe, alisema halmashauri hiyo imeweka historia kwa mara ya kwanza ya kutoa mkopo kupitia mapato yake ya ndani zaidi ya bilioni moja na kwa uwazi.

"Leo ninayo furaha kubwa sana kwa sababu katika jambo ambalo Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akilisema kwenye vikao na kwa maelekezo yake ndoto zake ni kuona kwamba kuna siku moja maalum yenye uwazi na kusanyiko la pamoja lakini kupitia jimbo langu Mkurugenzi Peter Nyaja amekuwa mfano wa kwanza kuitisha vikundi vyote na kutoa mikopo kwa uwazi kwa zaidi ya bilioni moja," alisema Dugange.

**"Na kikundi kikishindwa hili niliseme wazi kikishindwa kurejesha zipo sheria ambazo zimetungwa kwa ajili ya kukiwajibisha hicho kikundi," alisema Mwansasu.**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Wang'ing'ombe, Agnetha Mpangile, alipongeza kundi la wanawake kwa kuwa waaminifu kwa kukopa na kufanya marejesho kwa wakati bila ya usumbufu wowote na kuwataka kuendelea kuwa na ushirikino na umoja .

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Wang'ing'ombe, Dk. Peter Nyanja, alisema kwa muda wote ambao mikopo haijatolewa halmashauri hiyo imekusanya fedha zaidi ya shilingi bilioni moja na milioni 500 lakini leo utatoa mikopo ya shilingi bilioni moja na milioni 89 kwa awamu ya kwanza na awamu ya pili wanategemea kutoa mwezi Machi mwaka 2025 baada ya kuwa wamekusanya ili watoe mikopo yenye tija.

Mmoja wa wanufaika wa mikopo hiyo, Lupiana Kitaponda, aliishukuru serikali kwa kurudisha mikopo ya asilimia 10 kwa sababu walijua haitarudi tena na kueleza kuwa fedha hizo zitasaidia kukuza biashara zao.



Kamanda wa Polisi mkoa wa Shinyanga Janeth Magomi akizungumza na wananchi wa kata ya Mhongolo Halmashauri ya Manispaa ya Kahama (hawapo pichani), wakati akizindua kituo cha polisi kata ambacho wananchi walichangishana fedha kila kaya na kukodisha nyumba ambayo inatumika kama kituo cha polisi ili kukabiliana na wahalifu. **PICHA: SHABAN NJIA.**

# Wataka serikali kuzibana kampuni za kigeni

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

WAFANYABIASHARA mkoani Njombe wameiomba serikali kudhibiti kampuni za kigeni zinazofanya biashara ya kununua malighafi husussani parachichi huku zikiwa zimefungua akaunti za fedha za nje ya nchi badala ya za ndani ili kunusuru upotevu wa mapato.

Waliyasema hayo juzi wakati wa kikao kati ya wafanyabiashara na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwamba upotevu wa fedha za kigeni unasababishwa na kampuni hizo ambazo zinafungua akaunti za biashara nje ya nchi huku nchini wakifungua akaunti ndogo kwa ajili ya kulipa wafanyakazi pekee.

Walisema serikali itoe agizo kwa kampuni hizo kufungua akaunti zote Tanzania ili kunusuru fedha za kigeni na mapato yanayolipwa katika taifa lingine.

"Kwa mfano biashara ya parachichi kampuni za Kenya ziko karibu 26 hapa Njombe na maeneo mengine , kama biashara inalipa kwa nini kampuni zetu haziwezi kufanya kazi ni kwa sababu wale wana mwanya wa kukwepa kodi kwa kuwa zile fedha zinapoingia haziji kwetu," alisema Humphrey Milinga.

Mfanyabiashara Angelus Nziku aliomba kiwango cha ushuru na mrundikano wa tozo kwenye biashara ya hoteli na viwanda kupunguzwa ili kukuza sekta ya biashara na uwekezaji nchini.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipa Kodi (TRA) Richard Kayombo alisema maoni yote yatafanyiwa kazi kwa sababu mingine ni ya kiutendaji, kisheria na ya kisera hivyo kuwataka wafanyabiashara kuendelea na uzalishaji wakati serikali ikiendelea kushughulikia matatizo hayo.

Meneja wa TRA Mkoa wa Njombe, Specioza Owure, alisema mwaka 2024 lengo ni kukusanya Sh. bilioni 35.817 na kuanzia Julai hadi Novemba, mwaka huu, wamekusanya Sh. bilioni 14.155.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Mkoa wa Njombe, Sifael Msigala, aliishukuru serikali kuondoa zaidi ya kodi 400 huku pia akiomba mrundikano wa tozo kwenye biashara ya hoteli na viwanda kupunguzwa.

# Watakiwa uvumilivu kukabiliana na ukatili

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JAMII mkoani Njombe, imetakiwa kuwa na moyo wa ustahimilivu katika kuyakabili mambo yanayoweza kuchochea ukatili wa kijinsia na mauaji mkoani humo.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkurugenzi Uenezi, Vijana na Michezo, Jonson Mgimba kutoka Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA) wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa maktaba ya wilaya ya Njombe.

Alisema jamii inapaswa kupokea elimu inayotolewa ili kuwajenga kisaikolojia huku akieleza namna SMAUJATA inavyoshirikiana na serikali katika kukomesha matukio hayo.

"Sisi tumeamua kusimama kupiga kelele kupinga aina ya ukatili ambao unajitokeza kwenye jamii yetu, tumeona tuje tulizungumzie jambo ambalo ndani ya miezi miwili limeshika kasi sana katika nchi yetu la mtu kutekwa wengi tunalitazama sana hili kwenye muktadha wa kisiasa," alisema Mgimba.

Mgimba alifafanua kuwa: "Kuna ukatili mkubwa sana ambao umekuwa umejitokeza katika matukio hayo ikiwemo ukatili wa kingono, kibiashara na aina nyingine."

Pia alisema kutokana na takwimu kuonyesha kuwa kundi la vijana ndilo limeathirika zaidi na vitendo vya ukatili wamejipanga kuanza kutoa elimu.

"Tunapozungumza suala la ukatili kuna kundi fulani ambalo linaguswa kwa sehemu kubwa sana nalo ni kundi la vijana, hii ni sehemu ambayo ukatili mwingi hufanyika kwa hiyo hili ni kundi ambalo tunafikiri kuanza nalo mwaka ujao kwa tutafanya midahalo mingi sana nchini," alisema Mgimba.

Mmoja wa wakazi mkoani Njombe, Niko Mchirwa, alisema kuna sababu zilizochangia kuongezeka kwa vitendo vya ukatili mkoani humo ikiwemo suala la kutojaliana migogoro ya kimapenzi.

"Ukatili mimi ninavyoona wivu wa kimapenzi unawafanya watu wengi sana wafanyiwe ukatili pamoja na imani na kishirikina lakini pia watu kutojali matatizo ya wengine huo nao ni ukatili kwa hiyo mimi kama mwananchi nashauri jamii ijifunze kujali wenzao wanapohisi kuna dalili zozote za ukatili mtu anataka kufanyiwa itatusaidia kupunguza haya matukio," alisema Mchirwa.

Kutokana na vitendo vya ukatili, yakiwamo mauaji kuongezeka kwa kipindi cha mwaka 2024 katika mkoa wa Njombe, Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka, ametoa waraka ambao ameuelekeza usomwe kwenye makanisa na misikitini.



# Waziri asisitiza hifadhi Mji Mkongwe

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman, amesema Mji Mkongwe wa Zanzibar, unapaswa kulindwa na kuhifadhiwa kwa kuwa ni moja ya maeneo machache yaliyopewa hadhi ya kuwa urithi wa kidunia mwaka 2000.

Suleiman alisema hayo wakati akiweka jiwe la msingi la bustani ya Afrika House visiwani Zanzibar ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema kutokana na historia yake ya kipekee, usanifu wake wa kuvutia na urithi wake wa kitamaduni usio na kifani, kuna kila sababu ya watu wa Zanzibar kuendeleza urithi huo.

Katika eneo hilo la Shangani, alisema ni sehemu ambayo ni chimbuko la Mji Mkongwe ambalo limebeba historia ya kipekee inayoakisi zama za biashara, utamaduni wa asili na harakati za maendeleo.

Alisema Bustani ya Africa House ni sehemu muhimu ya maisha ya kijamii na kitamaduni ya wakazi wa Shangani na wageni wa Zanzibar hasa watalii wanaokuja visiwani Zanzibar.

"Bustani hii imekuwa ikitumika kwa mikusanyiko ya kijamii, matamasha na mapumziko kwa wakazi na watalii wanaotembelea Mji Mkongwe," alisema Waziri Harous.

Waziri huyo alisema eneo hilo liliachwa kwa miaka mingi bila kushughulikiwa na kusababisha kuta za kingo za bahari kuvunjika na bustani kupoteza mvuto uliokuwapo awali.

Alisema katika kuimarisha mandhari ya mji huo, serikali kati ya mikakati yake ni kuyafufua maeneo kama hayo ili kujenga ustawi mzuri wa mazingira na watu wake.

**"Kama ilivyoelezwa na kuoneshwa katika michoro, eneo hili litakuwa ni la kale lililochanganyika na mambo ya kisasa na hii ni katika ile ile dhamira ya uanzishwaji wa**

"Kama ilivyoelezwa na kuoneshwa katika michoro, eneo hili litakuwa ni la kale lililochanganyika na mambo ya kisasa na hii ni katika ile ile dhamira ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Mji Mkongwe ambayo ni uhifadhi na uendelezaji," alisema.

Alisema eneo hilo pia litakuwa na boti ambazo zitapeleka wageni visiwani na kuepukana na madhara ambayo yanaweza kutokea kwa kukosa miundombinu ya kufikia vyombo vya usafiri.

Mbali na faida ambazo zitapatikana baada ya kukamilisha mradi huu, pia kungalia uwezekano wa kuanzisha safari za baharini kuwapeleka wageni katika pembe nyingine za kisiwa kama vile Nungwi na kwingineko kwa kupitia boti zitakazokuwepo katika mradi huo ili kutanua wigo katika sekta ya utalii nchini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema serikali imeamua kwa makusudi kuyaimarisha maeneo yote ya kihistoria kususani Mji Mkongwe kwa lengo la kulinda ,kuhifadhi na kutunza alama za kihistoria.

Alisema wizara yake kupitia mamlaka ya uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe, imeendelea kujikita katika kuhakikisha utalii katika eneo hilo. "Eneo hili la urithi wa dunia linaleta tija kubwa na linatekeleza na kufuata vigezo vyote vya urithi wa miji ya kihistoria duniani," alisema Jumbe.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, Mhandisi Ali Said Bakar, alisema eneo hilo hadi kukamilika kwake, litakuwa limegharimu Dola za Marekani 800,000.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar , Othman Masoud Othman (kulia) akimsikiliza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhandisi, Hamad Yusuf Masauni alipokwenda kujitambulisha kwake hivi karibuni.
**PICHA: ROBERT HOKORORO**

# SMZ kujenga barabara zote kiwango cha lami

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imedhamiria kuzitengeza barabara zote kwa kiwango cha lami ili kuimarisha shughuli za kiuchumi kwa wananchi wake.

Waziri wa Habari, Vijana, Sanaa na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema hayo jana wakati akifungua barabara Mchanga Mle, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kuwapo kwa miundombinu mizuri ya barabara za mijini na vijijini kwa upande wa Unguja na Pemba ni moja ya njia za kurahisisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa wananchi wote wa Zanzibar .

Waziri huyo alisema serikali itahakikisha barabara zote za Zanzibar zinajengwa kwa kiwango cha lami na zinakuwa katika hali nzuri muda wote kwa kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara.

Pia alisema barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 4.5 inayounganisha barabara kuu kutoka mjini kwenda Kizimkazi, Makunduchi, itawanufaisha pia wananchi wa karibu wa maeneo hayo.

"Ujenzi wa barabara hii unaweza usione kwa vipi mwananchi wa kawaida ananufaika na ujenzi wake lakini kwa mwananchi unamgusa hasa kwa wakulima na wasafirishaji," alisema Waziri Tabia. Alisema kabla ya ujenzi wa barabara hiyo, hali ilikuwa mbaya na haipitiki, hivyo kusababisha usumbufu mkubwa kwa wafanyakazi na wageni waliokuwa wakifika makazi yao.

Pia alisema hali hiyo ilisababisha uongozi wa hoteli ya Residence kupeleka malalamiko serikalini ya kujengwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami na ulikuwa tayari kuchangia gharama za ujenzi.

Waziri huyo alisema serikali itazijenga barabara zote ambazo zinahitaji kujengwa katika mikoa yote Unguja na Pemba, hivyo wananchi wanaoishi maeneo ambayo bado ujenzi wake wa Barabara, wanatakiwa kuwa wavumilivu na serikali iko mbioni katika ujenzi huo.

Waziri Tabia alisema mafanikio makubwa yamepatikana toka Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 ya kuimarisha miundombunu ya barabara. Alisema mafanikio hayo ni matokeo ya juhudi za wananchi za kuunga mkono serikali kwa kila hatua katika kuwaletea maendeleo.

# Waahidi kulipa kodi kwa wakati

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA wa kampuni za mafuta Zanzibar wamesema wataendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha kodi zao zinalipwa kwa wakati uliowekwa ili kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato nchini.

Waliyasema hayo wakati walipotembelewa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), ikiwa ni mwezi wa shukrani na furaha kwa walipakodi hao katika maeneo ya Mtoni na Mangapwani.

Walisema ili serikali iweze kutekeleza mipango yake ya maendeleo lazima kodi zilipwe kwa wakati ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli hizo.

Mkaguzi na Msimamizi wa Hesabu ya Mafuta katika kituo cha Bohari Kuu ya Mafuta cha Mangapwani, Muhamed Ameir Hamid, alisema nchi yoyote duniani haiwezi kuendeshwa bila kodi, hivyo kuna haja kwa wafanyabiashara kuongeza jitihada za kuhakikisha wanalipa kodi kama ilivyopangwa na serikali.

Alisema kodi ina umuhimu mkubwa katika nchi, hivyo watahakikisha wanashirikiana na mamlaka hiyo kulipa kodi kwa wakati ili maendeleo ya Zanzibar yaweze kufika mbali kiuchumi.

Alitumia nafasi hiyo kuwashajihisha walipakodi wengine kuhamasishana kulipa kodi ili serikali iweze kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi ambao ndio walioiajiri serikali.

Mohamed Naushad Alam, ambaye ni msimamizi wa stoo kutoka kituo cha Zanzibar Petroleum Mtoni, aliahidi kuunga mkono jitihada za serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi wake kwa kulipa kodi kwa wakati.

Hata hivyo walitumia nafasi hiyo kuishukuru kuweka mwezi huo wa kuwashukuru walipakodi na kuahidi kwamba kampuni zao zitaendelea kushirikiana ili kuona Zanzibar inaendelea kupiga hatua kubwa za kimaendeleo.

Shaban Jafar Jumanne, Kamishna wa Idara ya Walipakodi Wakubwa ZRA, aliwapongeza wafanyabiashara wakubwa kwa kulipa kodi kwa wakati na kuiwezesha serikali kupata mapato.

Aidha alisema ZRA inatambua juhudi zinazochukuliwa na wafanyabiashara hao katika kuhakikisha maendeleo ya haraka yanapatikana kupitia kodi hizo.

Alibainisha kuwa, mamlaka hiyo ni lazima iwasaidie wafanyabishara kuwa katika hali nzuri ili waweze kulipa kodi zao kwa hiyari na kuisaidia serikali kufikia malengo yake ya kuwafikishia huduma muhimu wananchi ikiwemo afya, elimu na miundombinu.

"Hatutakiwi kuwa maadui bali tunatakiwa kushirikiana kwa pamoja ili nyinyi mfanye biashara zenu kwa amani na sisi tukusanye kodi zetu bila ya usumbufu wowote," alisema.

Shaaban, akizungumzia mwezi wa shukrani na furaha kwa walipa kodi alisema mamlaka imeandaa mwezi huo lengo likiwa ni kujenga mahusiano mazuri kati yao kwa maslahi mapana ya nchi.

Alimpongeza Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada anazozichukua za kuleta maendeleo makubwa kwa wananchi wa Zanzibar kupitia sekta mbalimbali ikiwemo afya, elimu, miundombinu ya barabara na sekta nyingine.

Alitumia nafasi hiyo kuwaomba wananchi kuendelea kumuunga mkono kwa kulipa kodi kwa hiari ili aendelee kuibadilisha nchi kimaendeleo.

Aliwataka wafanyabiashara kuwa mabalozi bora wa kulipa kodi ili kukuza maendeleo ya serikali.

# HABARI PICHA



Watoto wakifurahia kuogelea katika fukwe ya Coco Oyesterbay jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Mmoja ya wakazi wa jiji la Dar es Salaam akijiandaa kuogelea jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Watoto wakifurahia kuogelea katika fukwe ya Oyesterbay jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Mchungaji Msaidizi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Usharika wa Mlandege, Flora Chavala na Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Mlandege, Elia Konga (Kulia) wakimkabidhi cheti Joram Mwaikusa wakati wa ubatizo wa watoto 79 katika usharika huo mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Mchungaji Msaidizi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Usharika wa Mlandege Iringa Mjini, Flora Chavala akimbatiza mtoto Cailn Mwaikusa jana wakati wa ibada ya ubatizo kwa watoto 79 kanisani hapo. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Wakazi wa Kivule jijini Dar es Salaam wakichuna mbuzi kusherehekea Sikukuu ya Krismasi jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Polisi Kenya yakana kuhusika na utekaji

**NAIROBI,** Kenya

MKUU wa Jeshi la Polisi la Kenya, Inspekta Jenerali Douglas Kanja, amekanusha madai yanayohusisha polisi kuhusika na vitendo vya utekaji nyara wa watu unaoshika kasi nchini humo.

Katika taarifa yake iliyotolewa jana, Kanja alisema kuwa hakuna kituo cha polisi ambacho kinawashikilia watu walioripotiwa kutekwa.

"Ili kuondoa shaka, Polisi haihusiki na utekaji nyara wowote, na hakuna kituo cha polisi nchini ambacho kinawashikilia watu walioripotiwa kutekwa," alisema.

IGP huyo aliongeza kuwa Mamlaka Huru ya Kusimamia Polisi (IPOA) itachunguza utekaji nyara huo, na alitoa wito kwa wananchi wenye taarifa zozote muhimu kuhusu watu waliopotea kuripoti katika vituo vya polisi vilivyo karibu.

"Suala linalozungumziwa linapaswa kuchunguzwa na Mamlaka Huru ya Kusimamia Polisi na chombo kingine chochote kilicho huru. Tunatoa wito kwa mtu yeyote aliye na taarifa muhimu kuhusu mtu yeyote aliyepotea kuripoti katika kituo cha polisi kilicho karibu nawe." Alisisitiza.

Kauli ya mkuu huyo wa polisi inafuatia malalamiko kutoka kwa raia wa nchi hiyo kuhusu kuongezeka kwa visa vya utekaji nyara, hasa kwa vijana.

**BBC**

## Watu 38 wapoteza maisha kwenye ajali ya ndege

**ASTANA,** Kazakhstan

WATU 38 wamefariki dunia baada ya ndege waliyokuwa wakisafiria kutoka Azerbaijan, kuanguka Kazakhstan juzi.

Ndege hiyo ilikuwa ikitoka mji mkuu wa Azerbaijan, Baku kuelekea Grozny, katika jimbo la Russia la Chechnya.

Kulingana na taarifa zilizopatikana jana, ndege hiyo inayomilikiwa na Shirika la Ndege la Azerbaijan, ilianguka magharibi mwa Kazakhstan, ikiwa na jumla ya watu 67, wakiwemo abiria 62 na wafanyakazi watano.

Ndege hiyo aina ya Embraer 190, iliyokuwa ikielekea Grozny, Chechnya, ilitoka nje ya njia yake, kuvuka Bahari ya Caspian, na kuanguka karibu na mji wa Aktau, ambao ni kitovu cha mafuta na gesi.

Kwa mujibu wa rekodi za mifumo ya ufuatiliaji wa safari za ndege zilionesha ndege hiyo ikitoka nje ya njia yake kabla ya kuanguka.

Katika tukio hilo watu walionusurika walikuwa 29, wakiwemo watoto watatu, ambao wote wamelazwa hospitalini.

Abiria wa ndege hiyo ni 37 raia wa Azerbaijan, sita kutoka Kazakhstan, watatu raia wa Kyrgyzstan watatu na 16 Warusia. **DW**

# Dalili kutokea machafuko Syria yaanza kuonekana

**DAMASCUS,** Syria

SERIKALI mpya ya Syria, imesema wafanyakazi 14 wa wizara ya mambo ya ndani wameuawa na wengine 10 wamejeruhiwa katika shambulizi la kuvizia lililofanywa na vikosi vinavyomtii Rais aliyepinduliwa Bashar al-Assad.

Taarifa ilieleza kwamba mapigano hayo yalitokea karibu na bandari ya Tartous iliyoko katika bahari ya Mediterranean.

Ripoti zilisema kuwa vikosi vya usalama vilivamiwa wakati vikijaribu kumkamata ofisa wa zamani kwa tuhuma ya kutowajibika wakati akifanya kazi katika gereza maarufu la Saydnaya, karibu na mji mkuu Damascus.

Zaidi ya wiki mbili zilizopita, Assad alipinduliwa na vikosi vya waasi vinavyoongozwa na kundi la Kiislamu la Hayat Tahrir al-Sham (HTS).

Shirika la Haki za Kibinadamu la Syria (SOHR) lenye makao yake nchini Uingereza lilisema wanamgambo watatu pia waliuawa katika mapigano hayo.

SOHR iliongeza kuwa vikosi vya usalama baadaye vilidhibiti eneo hilo na kurudisha hali ya usalama.

Wakati huo huo, serikali ya Syria iliweka amri ya kutotoka nje usiku katika mji wa kati wa Homs kufuatia kuibuka kwa machafuko baada ya video inayodaiwa kuonesha shambulio kwenye hekalu la Alawite.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Syria, ilisema video hiyo ya zamani ilionesha wakati mashambulizi ya waasi yakianza mjini Aleppo mwishoni mwa mwezi Novemba, na kisha kutokea tukio hilo.

SOHR ilisema mtu mmoja aliyekuwa akiandamana aliuawa na watano walijeruhiwa.

Maandamano hayo pia yaliripotiwa katika maeneo mengine katika miji ya Tartous na Latakia, na mji alikozaliwa Assad wa Qardaha.

Alawites ni madhehebu ya wachache ambayo familia ya Assad inatoka.

Katika madhehebu hayo wapo wasomi, wanasiasa na wanajeshi wa utawala wa zamani.

Mashambulizi makali yaliyoongozwa na HTS ambayo yalianza kutoka kaskazini-mashariki mwa Syria na kuenea nchi nzima yalihitimisha utawala wa zaidi ya miaka 50 wa familia ya Assad.

**BBC**



Ndege ya shirika la ndege la Azerbaijan iliyoanguka juzi karibu na uwanja wa ndege nchini Kazakhstan. **PICHA: IMAGO**

# Wafungwa 1,500 watoroka wavunja ukuta wa gereza

**MAPUTO,** Msumbiji

ZAIDI ya wafungwa 1,500 wametoroka katika gereza moja nchini Msumbiji, wakati nchi hiyo inakabiliwa na wimbi la maandamano yenye ghasia.

Wafungwa hao walitoroka baada ya kufanikiwa kuangusha ukuta wakati waandamanaji wakipambana na polisi nje ya gereza hilo.

Mkuu wa Polisi, Bernardino Rafael alisema watu 33 waliuawa na wengine 15 kujeruhiwa katika mapambano kati ya walinzi na waandamanaji.

Katika msako wa kuwatafuta wafungwa hao, 150 wamekamatwa tena na kurudishwa gerezani.

Maandamano hayo yalianza Jumatatu kupinga uamuzi wa mahakama ya juu ya Msumbiji iliyothibitisha ushindi wa chama tawala cha Frelimo, ambacho kimetawala tangu mwaka 1975.

Kamanda Rafael alisema makundi ya waandamanaji wanaoipinga serikali yalikaribia gereza hilo katika mji mkuu Maputo siku ya Jumatano na kusababisha wafungwa kuangusha ukuta na kutoroka.

Msumbiji imekumbwa na machafuko tangu kufanyika kwa uchaguzi ulioibua mzozo mwezi Oktoba.

Matokeo rasmi yalionesha mgombea urais wa chama tawala cha Frelimo, Daniel Chapo, alishinda.

Matokeo ya awali ya mwezi Oktoba yalisema Daniel Chapo alipata asilimia 71 ya kura zote dhidi ya mpinzani wake mkuu Venancio Mondlane, aliyepata asilimia 20.

Katika uamuzi wa makahama hiyo, ulieleza mgombea wa chama tawala alishinda kwa asilimia 65 na Mondlane alipata asilimia 24.

**BBC**

# AZAM YATAMBA KUICHAPA JKT TANZANIA BILA HURUMA

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Azam FC kinatarajia kuikaribisha JKT Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam huku kikitamba kitawachapa Maafande hao pale pale 'walipopigwa' na Simba katika mchezo wao uliopita.

JKT Tanzania imetoka kupoteza mechi dhidi ya Simba, ikifungwa bao la dakika za lala salama kwa njia ya penalti iliyofungwa na Jean Ahoua.

Azam itakuwa na kazi moja tu kuhakikisha inapata pointi tatu na kufikisha pointi 36 kama Yanga, lakini iwapo kama inataka kupaa hadi nafasi ya pili ina kazi 'ngumu' ya kuifunga JKT Tanzania mabao zaidi ya 6-0.

Wanalambalamba wataingia uwanjani wakiwa na rekodi nzuri na kucheza michezo 10 bila kupoteza, ikishinda tisa na sare moja.

Timu hiyo haijapoteza mchezo wowote tangu ilipochapwa mabao 2-0 dhidi ya Simba, Septemba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.

Kocha Mkuu wa Azam, Rachid Taoussi, alisema wana nia moja tu ya kuendeleza ushindi kwao na vipigo kwa wapinzani, ingawa wanafahamu wanakwenda kukutana na mpinzani mgumu.

Kocha huyo alisema JKT Tanzania ni timu ambayo pamoja na kuonekana haifungi mabao mengi, lakini ina walinzi wazuri na hawaruhusu mabao kirahisi.

"Nia yetu ni kushinda mchezo, tumeshinda michezo tisa mpaka sasa na huu kama tukishinda utakuwa wa 10, nakiamini kikosi changu ambacho kwa sasa kimeimarika sana na wanacheza vile ambavyo nahitaji, lakini tunakwenda kucheza mechi ngumu, JKT Tanzania ni timu nzuri na ngumu sana kufungika," alisema kocha huyo raia wa Morocco.

Naye Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally, alisema baada ya kupoteza mchezo dhidi ya Simba wamesahau yaliyopita na sasa wamejipanga kucheza mechi hii ambayo wanaamini itakuwa ngumu huku wakishuka dimbani baada ya siku chache kupita.

"Tunakwenda kucheza mechi nyingine ngumu ndani ya siku chache, hata hivyo tumejipanga kuhakikisha tunafanya vizuri, wachezaji wangu nimewaweka vizuri kisaikolojia, naamini watafanya kile nilichowaeleza," alisema Ahmad.

Azam inakwenda kucheza mechi huo ikiwa katika nafasi ya tatu ya msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 33, nyuma ya mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 36 na Simba iliyo kileleni ikiwa na pointi 37 kibindoni.

JKT Tanzania itaingia dimbani ikiwa na pointi zake 19, ikishika nafasi ya nane katika msimamo wa Ligi Kuu Bara yenye timu 16 kutoka mikoa mbalimbali.



Golikipa wa IBG FC ya jijini Dodoma, Hassan Ibrahim (kulia), akidaka mpira kuokoa hatari langoni mwake katika mechi ya kirafiki dhidi ya timu ya kituo cha JMK Park iliyochezwa kwenye uwanja wa kituo hicho kilichoko Gerezani, Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mashujaa kamili kuivaa Dodoma Jiji

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Mashujaa FC kimewasili salama jijini Dodoma tayari kwa ajili ya kuwakabili wenyeji Dodoma Jiji katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mashujaa FC, Abdallah Mohamed 'Bares', alisema wachezaji wake wana morali ya juu kuelekea mchezo huo ingawa wanafahamu hautakuwa mwepesi.

"Tunashukuru tumefika salama kwa sasa tunaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo huo, malengo yetu ni kupata pointi tatu muhimu,' alisema Bares.

Kocha huyo alisema mechi zote za ligi hiyo ni ngumu na hakuna timu ya 'kubeza' kwa sababu kila moja imejipanga kusaka matokeo chanya.

Aliongeza morali ya kila mchezaji ipo juu na kusema watadai mchezo huo unatarajiwa kuwa mgumu na wenye upinzani hivyo wanapaswa kucheza kwa tahadhari.

"Nimewaambia wachezaji wacheze kwa tahadhari watakapokuwa na mpira ili mpinzani wetu asipate nafasi ya kutufunga kwa urahisi, najua haitakuwa mechi rahisi kwa sababu kila timu inataka kufikia malengo yake," kocha huyo alisema.

Aliongeza anatarajia kuongeza wachezaji ambao wataleta ushindani ndani ya timu hiyo katika dirisha dogo la usajili kwa sababu mipango yao ni kumalizka msimu kwenye nafasi za juu.

## Ligi Kuu Wanawake kuendelea tena leo

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi, Simba Queens ya Dar es Salaam wanatarajia kuwavaa Bunda Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Karume ulioko Musoma mkoani, Mara.

Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, aliliambia gazeti hili jana kila mechi msimu huu kwao ni sawa na fainali na hivyo wamekwenda Musoma kufuata pointi tatu muhimu.

Makanya alisema malengo yao ni kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa mwakani na ili kufikia mipango hiyo ni lazima wapambane kutetea ubingwa wanaoushikilia.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni Yanga Princess dhidi ya Gets Programu wakati Fountain Gate Princess itawaalika JKT Queens huku Ceasiaa ikiwafuta Alliance Girls huku Mashujaa Queens watapambana Mlandizi Queens kwenye Uwanja wa Kituo cha TFF, Kigamboni.

Simba Queens yenye pointi 19 ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na JKT Queens yenye pointi 17 na Yanga Princess ambayo imepoteza michezo mitatu inafuatia na pointi zake tisa kibindoni.

## CHANETA : Wanawake tusidharau mazoezi

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Netiboli Tanzania (CHANETA), kimewataka wanawake nchini kutoacha kufanya mazoezi kwa ajili ya kuimarisha afya na kujiweka imara, imeelezwa.

Mwenyekiti wa CHANETA, Devotha Marwa, alisema ni muhimu wanawake kufanya mazoezi kwa ajili ya kujiepusha na maradhi mbalimbali pamoja na kushiriki kwenye michezo.

"Mazoezi yana faida kubwa kwenye mwili wa binadamu. Ninawashauri wanawake wapende kufanya mazoezi kwa sababu yanajenga afya na vilevile huwaepusha na magonjwa mengi, mazoezi ni tiba pia," alisema Marwa.

Alisema anampongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi anazofanya kuhakikisha Tanzania inasonga mbele katika tasnia ya michezo.

"Rais Samia ni mwanamke ambaye anapambana kuona taifa letu linafika mbali katika nyanja za michezo, jambo ambalo linatupa nguvu sisi wadau.

Kwa sasa CHANETA tupo katika mchakato wa kuibua vipaji vya vijana kwa lengo la kupata timu bora ya taifa ya miaka ijayo," aliongeza kiongozi huyo.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**ZURICH YAMTAKA OYEDEJI**
KLABU ya FC Zurich imewasiliana na Arsenal kuuliza kuhusu upatikanaji wa mshambuliaji wa England, Nathan Butler-Oyedeji, mwenye umri wa miaka 21 ifikapo Januari. (***Football Insider***)

**MUANI KUTUA ARSENAL**
KLABU ya Paris St-Germain huenda ikaipa Arsenal nafasi ya kumsajili fowadi wao Randal Kolo Muani mwenye umri wa miaka 26.(***Standard***)

**DIBLING AWEKWA SOKONI**
KLABU ya Southampton inaweza kumuuza mchezaji wao chipukizi, Tyler Dibling, mwenye umri wa miaka 18, ikiwa watashuka daraja kutoka Ligi Kuu England, huku Manchester United na Newcastle United zikionyesha nia ya kumnunua kiungo huyo wa kati wa Uingereza. (***Football Insider***)

**POGBA HAJATUA CITY**
UVUMI ulioenea kuhusu kiungo wa zamani wa Manchester United na Juventus, Paul Pogba, mwenye umri wa miaka 31, ameonekana kwenye uwanja wa mazoezi wa Manchester City haukuwa wa kweli. (***Fabrizio Romano***)

**FAGIOLI AITAKA SPURS**
WEST Ham, Fulham, na Crystal Palace zote zinamfuatilia kiungo wa Juventus, Nicolo Fagioli, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia mwenye umri wa miaka 23 anavutiwa na Tottenham Hotspur. (***Tuttosport***)

**SESKO ATAJWA CHELSEA**
CHELSEA inafikiria uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Slovenia, Benjamin Sesko, mwenye umri wa miaka 21. (***TeamTalks***)

**HJULMAND KITAELEWEKA**
BOSI wa West Brom, Carlos Corberan na kocha zamani wa Denmark, Kasper Hjulmand, ni miongoni mwa wawanaowania kuchukua nafasi ya Russell Martin huko Southampton, lakini bosi wa muda Simon Rusk atabakia kuinoa timu hiyo kuelekea mechi dhidi ya Fulham itakayochezwa keshokutwa. (***Sky Sports***)

**DUBRAVKA ANUKIA SAUDIA**
KLABU ya Saudi Arabia ya Al-Shabab inavutiwa na dili la bei iliyopunguzwa kwa mlinda lango wa Newcastle United na Timu ya Taifa ya Slovakia, Martin Dubravka, mwenye umri wa miaka 35. (***I***)

**DANSO SOKONI JANUARI**
KLABU ya Wolves inaweza kulenga uhamisho wa Januari kwa mlinzi wa kati wa Austria, Kevin Danso, mwenye umri wa miaka 26, ambaye Lens inaweza kutaka kumuuza. (***L'Equipe***)

**AKLIOUCHE AIWAZA BARCA**
KIUNGO mshambuliaji wa Monaco na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Maghnes Akliouche, mwenye umri wa miaka 22 amesema angependa kuichezea Barcelona katika maisha yake ya soka. (***Sport***)

**NELSON KUONDOKA ARSENAL**
WINGA wa Arsenal, Reiss Nelson (25), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Fulham - ataruhusiwa kuondoka kwa washikabunduki hao msimu ujao kwa sababu kuna uwezekano mchezaji huyo hatakuwa sehemu kubwa ya mipango ya Mikel Arteta katika siku zijazo. (***Mail Plus***)

**ROBINS AIKACHA MILLWALL**
BOSI wa zamani wa Coventry, Mark Robins, amekataa fursa ya kuzungumza na klabu nyingine ya Championship, Millwall kuhusu nafasi yao ya ukocha. (***South London Press***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SLOT: HATUDHARAU KLABU YOYOTE EPL

**●●●Kocha huyo asema kila mechi msimu huu ni ngumu na wataikabili...**

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Mkuu wa Liverpool, Arne Slot, amesema hawezi kuidharau timu yoyote licha ya wao kuongoza katika msimamo wa Ligi Kuu England inayoendelea, imeelezwa.

Liverpool iko mbele kwa pointi nne dhidi ya Chelsea inayoshika nafasi ya pili ikiwa imecheza mechi pungufu baada ya ushindi wa mabao 6-3 dhidi ya Tottenham Hotspur Jumapili iliyopita.

Kikosi cha Slot kimepoteza mechi moja tu kati ya 16 za ligi hiyo msimu huu na jana Alhamisi kilikuwa kwenye nafasi ya kuendeleza kiwango chake kilipoikaribisha Leicester City.


**Timu hiyo inayonolewa na Kocha, Ruud van Nistelrooy, iko katika nafasi ya 17 kwenye msimamo, ikiwa imeshinda mara tatu pekee kati ya michezo 17 ya ligi waliyocheza msimu huu.**

"Nadhani jambo chanya ni timu zinazoshika nafasi ya chini katika msimamo wa ligi mara nyingi hupoteza michezo, lakini hatutakiwi kuidharau timu yoyote," alisema Slot.

"Sasa alikuwa na matokeo magumu mawili mfululizo, timu hizi zote ni maalum kwenda Anfield na wanajua wakienda Anfield lazima wawe kwenye ubora wao ili wasitudharau kamwe.

"Hivyo sisi tutaipa kipaumbele sawa timu yoyote tutakayokutana nayo kwa sababu hakuna wa kumdharau na zote zinaonekana kuwa fiti sana.

"Licha ya kuwa tupo kileleni katika msimamo haifai kusema sisi ni bora zaidi kuliko wao, lazima tupambane katika kila mechi ili tuweze kushinda na kuonyesha ubora wetu."




# BAYERN MUNICH YAMWONYA JOSHUA KIMMICH

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich imeripotiwa kumwonya kiungo wake wa kati, Joshua Kimmich, na inataka jibu kuhusu ofa yao ya mkataba mpya ifikapo Januari.

Kimmich anakaribia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake kwa miamba hao wa Bavaria na tayari ametambuliwa kama uwezekano wa uhamisho wa bure katika majira ya joto.

Tayari Manchester City na Barcelona zote zikihusishwa na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 hivi karibuni alisema atafanya uamuzi kuhusu mustakabali wake ifikapo Januari, lakini kwa mujibu wa Sky Sports ya Ujerumani, hiyo inaweza isitoshe haraka kwa Bayern Munich.

Bayern Munich inataka jibu kutoka kwa Kimmich mapema Januari, wakifahamu vyema kuchukua nafasi ya mtu muhimu kama huyo kutahitaji miezi ya utafiti na maandalizi.

Viongozi wa klabu hiyo wabainisha hadharani wanataka Kimmich awe msingi wa siku za usoni na wanataka kumpa mkataba mpya, lakini kiungo huyo bado hajafanya uamuzi.

Mara tu Januari itakapofika, Barcelona na Manchester City wanaweza kuwasiliana na Kimmich na kujadili kuhusu mkataba mpya ambao utaongeza shinikizo kwa Bayern Munich.

Kimmich sio kiungo pekee wa Bayern Munich anayevutiwa na timu za Ligi Kuu England, kwa sababu Manchester United pia imeripotiwa pia kumwania nyota huyo.

# Oscar kurejea Sao Paulo




**SAO PAULO,** Brazil

MCHEZAJI Oscar atarejea katika klabu yake ya zamani ya São Paulo kwa mkataba wa miaka mitatu, timu hiyo ya Ligi Kuu Brazil, imesema.

Kiungo wa zamani wa Chelsea, Oscar, ambaye aliichezea Timu ya Taifa ya Brazil mara 48 kati ya mwaka 2011 na 2016, ametumia misimu minane iliyopita akiwa na Klabu ya Shanghai Port, akishinda taji la Ligi Kuu China mara tatu.

"Nina furaha kurejea Brazil na kuichezea São Paulo, ambayo ni klabu niliyoanzia, nilipata msingi wangu na nilikokulia," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33.

Oscar alifunga mabao 38 katika mechi 203 alizoichezea Chelsea na kunyanyua mataji ya Ligi Kuu England, Kombe la Ligi na Ligi ya Europa katika kipindi chake cha miaka minne na nusu.

Alianza kucheza soka la kulipwa São Paulo mwaka 2008 na alijiunga na Internacional miaka miwili baadaye, hatua iliyosababisha mzozo mrefu wa mkataba kati ya klabu hizo mbili za Brazil.

# Disasi wa Chelsea anukia Bundesliga

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayer Leverkusen imewasiliana na beki wa Chelsea, Axel Disasi, kuhusu uwezekano wa uhamisho wa Januari, kwa mujibu wa ESPN.

Disasi anaonekana kuwa chaguo la tano la beki wa kati wa Kocha, Enzo Maresca, nyuma ya Levi Colwill, Wesley Fofana, Benoit Badiashile na Tosin Adarabioyo, na amefanikiwa kucheza mechi nne pekee kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

Kwa mujibu wa Sky Sports, Disasi amechukizwa na nafasi yake ndogo na sasa anafikiria kuondoka Chelsea katika dirisha dogo la usajili la Januari.

Inasemekana hali yake imevutia macho ya Bayer Leverkusen, ambao wamefikia kuzungumzia uhamisho wa majira ya baridi huku wakitoka jasho kutokana na uwezekano wa kuondoka kwa nahodha, Jonathan Tah, ambaye anaingia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake.

Disasi pia anavutiwa na Juventus, lakini timu hiyo ya Serie A inaweza tu kutoa mkataba wa mkopo wa awali - jambo ambalo linaweza lisiwe na faida kwa Chelsea.

Maresca, kwa upande wake, amesisitiza nia yake ya kutaka kumbakiza mchezaji huyo kikosini, lakini akakiri wale wanaohangaika kwa kukosa muda wa kucheza lazima waamue kama wana furaha kuendelea kupigania mustakabali wao.



## CAF yaibeba Simba Tunisia

INATOKA UKURASA 24

Nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo inashikiliwa na Yanga yenye pointi 36 ikifuatiwa na Azam FC yenye pointi 33, lakini ina uwiano mzuri wa magoli ya kufunga na kufungwa ukilinganisha na Singida Black Stars.

## Ramovic aanika siri ya ushindi Yanga SC

INATOKA UKURASA 24

waliokuwa wakishambulia kwa kushtukiza na kuwapa 'tabu' wakati fulani.

Mabao ya Yanga katika mchezo huo wa juzi yalifungwa na Clement Mzize, aliyetupia mawili, Prince Dube na Stephane Aziz Ki, kila mmoja akifunga goli moja.

Ramovic, tayari ameiongoza Yanga kushinda michezo minne ya Ligi Kuu, akianzia dhidi ya Namungo aliposhinda mabao 2-0, Mashujaa FC (mabao 3-2), Prisons na Dodoma Jiji kila timu ikipata kipigo cha mabao 4-0.

Hata hivyo, ushindi huo unaendelea kuwabakisha katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi baada ya kufikisha pointi 36, nyuma ya vinara Simba wenye pointi 37.

Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Mecky Maxime, alisema timu yake ilistahili kufungwa.

"Tumestahili kuadhibiwa, ukiangalia mabao yote manne ni wachezaji kutojiamini, kufanya makosa yale yale ya kujirudia na kuwapa mipira wachezaji wa Yanga, wanatufunga, kwa hiyo tutakaa chini tuangalia nini turekebishe na kama kuna nguvu inatakiwa iongezwe, yaani kusajili wachezaji kipindi hiki cha dirisha dogo, basi tuongeze," alisema kocha huyo.

Yanga itarejea tena uwanjani keshokutwa kuwakaribisha Fountain Gate na baada ya hapo itaanza maandalizi ya kuikaribisha TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo) kwa ajili ya mechi ya raundi ya nne ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa Januari 3, mwakani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

# SERENGETI BOYS, UGANDA HAPATOSHI FAINALI CECAFA

**Na Adam Fungamwangwo**

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), wanakutana na Uganda katika mechi ya fainali ya Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-17), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Hamza Nakivubo jijini Kampala, Uganda.

Serengeti Boys na Uganda zimefuzu kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-17), zitakazopigwa Machi, mwakani nchini Morocco.

Serengeti Boys ilifuzu fainali hizo baada ya kuitwanga Sudan Kusini mabao 4-0, shukrani kwa Hussein Mbegu, Abel Joasiah na Ng'habi Zamu huku Uganda Cubs, ikiwachapa Somalia magoli 4-1 katika michezo yao ya hatua ya nusu fainali.

Kocha Mkuu wa Serengeti Boys, Agrey Morris, amesema wachezaji wake wako kamili kwa ajili ya mchezo huo aliotabiri utakuwa mgumu.

"Tupo kamili, wachezaji wapo katika hali nzuri na morali ya hali ya juu kwa ajili ya mchezo huu, kila mmoja yupo tayari kufanya kile atakachoagizwa akipatiwa nafasi. Tunacheza mechi ya fainali, ni muhimu, tunaomba sapoti ya Watanzania ili tuchukue kombe hili.

Ni wazi haitakuwa mechi rahisi kwa sababu Uganda wana timu nzuri sana na watakuwa nyumbani, pamoja na hilo hatuwahofii, tutapambana," alisema nahodha huyo wa zamani wa Tanzania (Taifa Stars).

Naye mchezaji timu hiyo, Saleh Ally, aliwaahidi Watanzania wajiandae kuwapokea wakiwa wanarejea nyumbani na kombe.

"Tunawaahidi Watanzania mechi hii tutafanya kila linalowezekana ili turudi Tanzania na ubingwa, nasema hivyo kwa sababu wachezaji tumejipanga kuhakikisha tunashinda mechi hii," alisema mchezaji huyo.

Awali timu hizo zilikuwa pamoja katika Kundi A na mechi yao ya hatua hiyo ilimalizika kwa sare ya bila kufungana, lakini kila mmoja akipata ushindi dhidi ya yosso wa Kenya.

Kundi B katika mashindano hayo lilikuwa na Sudan Kusini, Somalia na Sudan.



Wachezaji wa Serengeti Boys wakifanya mazoezi ya mwisho kwenye Uwanja wa Philip Omondi ulioko Kampala, nchini Uganda ili kujiandaa na mechi ya fainali ya Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-17), dhidi ya wenyeji Uganda itakayochezwa leo jijini humo. **PICHA: TFF**

# Namungo: Dirisha dogo safi

**Na Adam Fungamwangwo**

WACHEZAJI wa Namungo FC, wamekiri usajili wa wachezaji wapya katika dirisha dogo limeongeza nguvu ndani ya kikosi chao na kusaidia kutopoteza mechi katika michezo yao mitatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa hivi karibuni.

Namungo imeshinda mechi mbili za ugenini na kutoka sare mara moja nyumbani na sasa imefikisha pointi 17 na kupanda hadi nafasi ya nane kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Nahodha wa Namungo, Erasto Nyoni, alisema hayo baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa mkoani, Manyara ambapo timu yao ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Fountain Gate.

Nyoni, ambaye ni beki wa kati, amesema hata wachezaji wa zamani wamefurahia ujio wa nyota hao wapya kwa sababu wameongeza nguvu kikosini tofauti na walivyokuwa awali.

"Kusema kweli wachezaji wapya waliosajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo wamekuja kuongeza nguvu kubwa katika kikosi, kinaonekana kuimarika, tunawashukuru sana na sisi waliotukuta tunawapa sapoti kubwa ndiyo maana unaona kuna mafanikio," alisema Nyoni.

Nyota wapya waliosajiliwa na Namungo mpaka sasa ni kiungo, Najib Mussa kutoka Singida Black Stars na mabeki waliorejea, Derrick Mukombozi na Emmanuel Charles.

"Ilikuwa mechi ya kisasi, katika mchezo wa mzunguko wa kwanza Fountain Gate walishinda kwetu na sisi tumekuja kuwafunga kwao, hiyo ni sehemu ya mchezo, nawashukuru wachezaji wangu kwa kazi kubwa walioifanya," Juma Mgunda, Kocha Mkuu wa Namungo, alisema.


# Michezo

Nipashe

Ijumaa Desemba 27, 2024




Bayern Munich yamwonya Kimmich UK. 22



Mshambuliaji wa Yanga, Prince Dube, akipiga shuti katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya 'Maafande' wa Tanzania Prisons iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam hivi karibuni. Yanga ilipata ushindi wa mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

## Ramovic aanika siri ya ushindi Yanga SC

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, Sead Ramovic, ametaja sababu inayowapa ushindi timu yake ni kufuatia wachezaji wake kucheza kwa kuzuia na kushambulia pamoja bila kutegeana katika mechi zao za hivi karibuni.

Ramovic ametoa kauli hiyo baada ya kupata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Dodoma Jiji katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi.

Kocha huyo alisema hali hiyo inasaidia kuondoka na pointi tatu muhimu lakini pia akiwaambia wanachama na mashabiki wa timu hiyo watafurahi zaidi pale wachezaji wake watakapokuwa na utimamu wa mwili kwa asilimia 100.

Alisema kwa sasa kikosi chake kinamudu zaidi kucheza mfumo anaotaka kipindi cha kwanza tu kwa sababu bado wachezaji hawajakuwa fiti kwa kiwango cha kutosha.

"Katika mfumo wangu nataka kila mchezaji akimbie, azuie wakati timu haina mpira na kushambulia wakati tuna mpira, tunazuia pamoja na tunashambulia pamoja.

Ukiangalia tumecheza michezo mitatu ndani ya siku saba, kwa hiyo wachezaji wangu wanatumia kipindi kimoja kuamua mechi, kama ukifuatilia utagundua tunafunga mabao mengi kipindi cha kwanza ambacho tunacheza kwa kasi na kufanya kama ninavyohitaji, hatufanyi hivyo kipindi cha pili kwa sababu tayari wanakuwa wameshachoka.

Lakini kwa bahati nzuri wana uwezo wa kuhimili mashambulizi, nadhani tunakwenda taratibu, tutaanza kucheza kwa kasi kwa dakika 90, mambo haya yatakuja hatua kwa hatua," alisema kocha huyo raia wa Ujerumani.

Hata hivyo aliisifia Dodoma Jiji akisema ni timu nzuri, yenye wachezaji wenye nguvu,

INAENDELEA UK. 23

# CAF yaibeba Simba Tunisia

## Ni baada ya CS Sfaxien kuhukumiwa kucheza bila ya mashabiki...

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), limetangaza kuifungia CS Sfaxien ya Tunisia kucheza mechi zake mbili za mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho bila mashabiki kufuatia vurugu walizofanya dhidi ya CS Constantine ya Algeria.

Katika mechi hiyo CS Sfaxien ikiwa mwenyeji ilifungwa bao 1-0, mashabiki wao walitupa mafataki, jambo ambalo limepigwa marufuku na wasimamizi hao wa soka Afrika.

CAF pia imewatoza CS Sfaxien faini ya Dola za Marekani 50,000 (sawa na Sh. milioni 119).

Adhabu hiyo ya CS Sfaxien, itainufaisha Simba ambayo itasafiri kwenda Tunisia kucheza mchezo wa raundi ya nne dhidi ya timu hiyo, mechi itakayofanyika Januari 5, mwakani.

Mechi nyingine ambayo CS Sfaxien itacheza bila mashabiki wake ni Januari 19, mwakani pale itakapowakaribisha Bravos do Maquis ya Angola.

Hata hivyo, timu hiyo huenda ikakumbana na adhabu nyingine kutokana na vurugu zilizotokea katika mechi dhidi ya Simba iliyochezwa Desemba 15, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, wenyeji wakishinda mabao 2-1.

Mashabiki na wachezaji wa CS Sfaxien walifanya vurugu katika mechi hiyo kufuatia mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis, kufunga bao dakika za 'jioni'.

Baada ya bao hilo lililoipa Simba ushindi kufungwa, kulitokea vurumai kubwa ndani ya uwanja, ambapo benchi la ufundi na baadhi ya wachezaji walimvamia mwamuzi wa mchezo, huku jukwaani nako kukiwa na tafrani kati ya mashabiki wa timu hiyo pamoja na wenyeji na kupelekea uharibifu wa viti kung'olewa.

Watunisia hao waliondoka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa huku wakiahidi watalipa kisasi watakapokuwa nyumbani kwao.

Kucheza bila mashabiki inaonekana ni faraja kwa Simba kwa sababu pamoja na itakuwa imelainishiwa mchezo kutokana na wenyeji kukosa faida ya kushangiliwa ili kuwaongezea hamasa wachezaji wao.

Wakati hayo yakiendelea, Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu, amewekа wazi kikosi chao kitaongezewa nguvu ya wachezaji wapya kipindi cha dirisha dogo la usajili kwa ajili ya kukiimarisha.

Mangungu alisema uongozi unaendelea kukamilisha mazungumzo na baadhi ya wachezaji inaowahitaji ili kuifanya Simba iwe na nguvu zaidi katika michuano ya kimataifa na Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Ni kweli tunatarajia kuongeza wachezaji, kwa tathimini ya kocha kuna mahitaji, tumeashaanza kuzungumza na baadhi ya wachezaji wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kujiunga na timu yetu, mambo yatakapokuwa tayari tutawatangazia," alisema Mangungu.

Tayari Simba imeshakamilisha usajili wa winga, Elie Mpanzu, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), ambaye tayari ameshaanza kutumika kwenye mechi za Ligi Kuu Bara.

Wakati huo huo, kikosi cha Simba kinatarajiwa kuondoka leo jijini ili kuelekea Singida kwa ajili ya mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Black Stars utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Liti mkoani humo.

Simba yenye pointi 37 ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara watakutana na Singida Black Stars ambayo ina pointi 33 iko nafasi ya nne katika msimamo imekuwa na msimu mzuri.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >